SUPA JACKPOT
TZS. 1,099,164,188
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Ndumbaro** apendekeza utafiti ufanyike makosa uhujumu uchumi vigezo kisheria

UKURASA 4




UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Aprili 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581270

www.ippmedia.com

The G… digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# NGO 29 kikaangoni tuhuma ushoga

UKURASA 2

## YALIYOMO



UKURASA WA 3

### SAMIA APANGUA MABALOZI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemhamisha kituo cha kazi aliyekuwa Balozi...

UKURASA WA 5

### RASIMU MITAALA MIPYA, SERA YA ELIMU YAIVA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema rasimu za mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo...

UKURASA WA 19

### MAANDAMANO KENYA, DPP ATAKIWA KUELEZA

SHIRIKISHO la Wanahabari nchini Kenya, limetoa siku saba kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP) kutoa taarifa...




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akionyesha kitabu chenye mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, baada ya kuzindua jijini Dodoma jana. Kulia ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mpango akiri Tanzania kukabiliwa tatizo la ajira

UKURASA 3



## Aliyepata ajali mwendokasi adaiwa kupoteza kumbukumbu

UKURASA 2 & 4

**MICHEZO** YANGA SC MDOMONI KWA PYRAMIDS UK.24

**KATUNI** UK.6



Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kusenyi, wakiwa barabarani baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha kijijini hapo, Musoma Vijijini, mkoani Mara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyepata ajali ya mwendokasi adaiwa kupoteza kumbukumbu

**Na Mary Geofrey**

MAISHA mapya ya majeruhi wa ajali ya basi la mwendo wa haraka (mwendokasi), Osam Milanzi, baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini, yamegeuka kitendawili kwa ndugu, jamaa na marafiki kutokana na kupoteza kumbukumbu.

Machi 20, mwaka huu, Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), ilimruhusu Milanzi, kurejea nyumbani baada ya afya yake kuimarika, kutokana na ajali aliyoipata Februari 22, mwaka huu.

Wiki mbili tangu Osam atoke hospitalini hakumbuki kama alipata ajali na ndugu wameshindwa kumueleza jambo hilo kutokana na kumbukumbu zake kutoka na kurejea.

Mdogo wa Milanzi, Shaban Milanzi, akizungumza kwa kina na Nipashe kuhusu siku 14 za kumuuguza nyumbani kaka yake, alisema hawaoni shida kukaa naye isipokuwa wasiwasi wao upo kwenye kurejea kwa fahamu zake.

"Tunasubiri kesho (leo) ifike kwa hamu turejee MOI kwa ajili ya kliniki ya kwanza nafikiri madaktari wanaweza wakatuambia tunafanyaje, maana Osam ni baba wa familia na anategemewa, sasa kama hana tena kumbukumbu inakuwaje," alihoji Shaban.

Amesema jambo linalowatatiza ni kuwa anakumbuka watu vizuri, lakini baada ya muda kumbukumbu zake zinapotea na kuanza kuchanganya mada.

"Unampa pole, anajibu asante Mungu atajalia nitapona, baada ya muda anajibu tena nani kawaambia naumwa nipo vizuri kabisa na mambo mengine anayozungumza nje kabisa na mada," alisema Shaban.

Shaban anatamani kufahamu kutoka kwa madaktari bingwa kama kaka yake atapona na kurejea katika hali yake ya zamani au la!



**MATIBABU NYUMBANI**

Mdogo wake Milanzi amesema wamekuwa wakiendelea na matibabu ya kumsafisha kidonda kila baada ya siku mbili au tatu katika maeneo alipoumia ikiwamo kichwani, kwenye paji la uso, kisogoni na kwenye paja.

"Tunatumia manesi wa hospitali za mtaani tu tunakubaliana anakuja anamsafisha na tunamlipa hela yake, kwa hiyo hatuwezi kusema ni kiasi gani tunatumia kwa sababu ni maelewano yanafanyika," alisimulia.

Alisema pia wananunua dawa za maumivu ambazo ameandikiwa na daktari ili kuhakikisha hali yake inarejea na kupona vidonda vyote.

Alisema kidonda kikubwa alichonacho ni kwenye paja ambalo limefungwa antena hali inayomsababisha asiweze kusimama mwenyewe.

"Ni mtu wa kulala kitandani na kumgeuza hivyo tunatakiwa tumfanyishe mazoezi kama tulivyoelekezwa na madaktari kwa sababu hata miguu yake haiwezi kusimama tena ni kama vile anajifunza upya," alisema Shaban.

Hata hivyo, wanaona maendeleo mazuri ya mgonjwa wao tofauti na alivyotoka hospitali kwa sababu sasa ameanza kujigeuza mwenyewe kitandani kidogo kidogo.

Shaban alisema hali ya mgonjwa inatia matumaini kwa sababu anaweza kuongea vizuri na yupo katika hali ya ucheshi isipokuwa kupoteza kumbukumbu.

**FAMILIA**

Shaban alisema Osam (38) ni mume wa mke mmoja na watoto watatu.

"Mmoja yupo kidato cha tatu Shule ya Sekondari Manzese, mwingine anasoma Shule ya Msingi Mianzini darasa la tano na wa mwisho anasoma chekechea," alisema.

Alisema mke wake amekuwa akikaa naye sasa kwa ajili ya kumuuguza wakati yeye ikimlazimu kutafuta fedha za kulisha familia na mahitaji mengine.

Kazi ya Shaban ni kuuza samaki wa kukaanga eneo la Mabibo Makutano, lakini biashara yake haiendi vizuri kutokana na mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Fedha za kumhudumia kaka yake wanachanga familia, ndugu, jamaa na marafiki na watu wenye mapenzi mema walioguswa na tukio hilo.

"Inabidi nijiandae kwa sababu ni wajibu wangu kumhudumia kaka yangu, siwezi kusema natoa fedha nyingi kumhudumia kwa sababu napata misaada kidogo kutoka kwa watu mbalimbali ambazo zinasaidia kuitunza familia yake na mgonjwa," alisema.

Shaban alisema anaweza kukusanya kati ya Sh. 70,000, Sh. 90,000 hadi Sh.100,000 kwa nyakati tofauti ambazo hutumia kulipa gharama mbalimbali za mahitaji anayotaka mke wake.

"Niwashukuru watu wanaoguswa moja kwa moja kunisaidia jambo hili, mimi siwezi kukaa nyumbani kumtunza kaka yangu inabidi nichakarike, lakini kama sio hii michango ni-

INAENDELEA UKURASA 4


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
03.04.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya ALHAMISI tarehe **06.04.2023** kampuni ya **CEVA INTERFREIGHT (T) LTD** itasafirisha magari tupu yenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Bandari ya Dar es salaam gari hizo zenye namba za usajili: **DS OOTG GP / NRB23609 NRB97300 / NRB15200**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 36.2** |
| **Upana** | - | **mita 4.3** |
| **Kimo** | - | **mita 4.6** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar es salaam** Kupitia **Morogoro Road.** Gari zitasafiri muda wa asubuhi ***(Kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117353702


# NGO 29 kikaangoni tuhuma za ushoga

**Na Halfani Chusi**

BARAZA la Taifa la Mashirika yasiyo ya kiserikali (NaCoNGO), limeanza kuyahoji mashirika 29 yasiyo ya kiserikali (NGO), dhidi ya tuhuma iliyoibuliwa na waziri wa zamani, Dk. Harrison Mwakyembe na baadaye kusambaa kwenye mitandao ya kijamii alizodai zinajihusisha na kampeni ya kueneza ushoga nchini.

Mwakyembe ambaye aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali kwenye serikali ikiwamo Waziri wa Katiba na Sheria, alitoa taarifa hiyo kwenye mkutano ulioandaliwa na viongozi wa dini kupinga mapenzi ya jinsia moja uliokuwa na kaulimbiu 'Tanzania bila ushoga inawezekana'.

Kwenye taarifa yake, alisema utafiti walioufanya kupitia tume aliyoiunda umebaini kuna mashirika 29 yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na vitendo vya kueneza mapenzi ya jinsia moja (ushoga), jambo ambalo ni kinyume na maadili ya kitanzania.

Kupitia tamko hilo lililogusa hisia za watu wengi na kuzua gumzo kwenye mitandao ya kijamii, Mwenyekiti wa NaCoNGO, Lilian Badi alisema baada ya kuona taarifa hiyo kuna hatua kadhaa walizichukua kukabiliana na kilichoibuliwa.

"Tumeyaita na kuanza kuyahoji hayo mashirika yaliyotuhumiwa na kufanya uchunguzi wa kina na tunamuhoji Dk. Mwakyembe ili tujue alifanyaje utafiti wake mpaka akabaini uwapo wa NGOs 29 zinazoshinikiza ushoga."

"Tulifanya kikao cha dharura cha kamati tendaji kujadili namna ya kuchunguza hali hiyo na kuweka maazimio ya utekelezaji, kufanya mawasiliano ya awali na mashirika yote yaliyotuhumiwa kupitia utafiti huo ikiwa ni maandalizi ya kuwafanyia uchunguzi pamoja na mahojiano ya kina," alisema Dk. Lilian na kuongeza:

"Hatua nyingine, tumeomba kukutana na kamati ya Dk. Mwakyembe ili tupatiwe taarifa yao itusaidie kuendeleza maoni yetu na juhudi tutakazozichukua kama viongozi wa sekta na NGO."

Alisema baada ya kukamilisha hatua hizo, wataandaa taarifa ya pamoja itakayoambatana na tamko kwa umma kuweka hadharani hatua watakazo zichukua.

Alitahadharisha kuwa ni vyema kutambua suala hilo ni mtambuka sio NGO pekee wanaohusika, hata serikali pia kupitia vyombo vyake, wabia wa maendeleo na makundi mengine ambayo hayajatajwa moja kwa moja na kwamba busara inahitajika katika kushughulikia sakata hilo.

"Tunataka kulinda jamii yetu, tuna kiu ya kubaki salama suala hili lipo kinyume cha maadili ya kitanzania, ni vyema tuungane pamoja kuliko kujigawa kama baadhi ya taarifa zilizosambaa zinamweleko wa kunyooshea vidole baadhi ya makundi."

Pia aliwataka wamiliki wa mashirika hayo kuepuka kuhukumu baadhi ya makundi au taasisi mpaka pale watakapokuwa na taarifa kamili au kuthibitika bila mashaka kama kundi fulani limehusika na kashfa hiyo.

Alisema ni vyema mjadala kuhusu suala hilo ungoje taarifa rasmi ya NaCoNGO, kuhusu hali halisi itakayotoa undani wa uchunguzi kwa mashirika yote yaliyohusika na tuhuma hizo, kisha taarifa yao itapelekwa katika bodi ya uratibu kupitia ofisi ya msajili wake iliyopo nchini.

## HABARI KITAIFA

# Mpango: Tanzania inakabiliwa tatizo ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amekiri kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Tanzania bado inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira, mitaala ya elimu isiyokidhi mahitaji ya soko la ajira pamoja na umaskini wa kipato kwa wananchi wake.

Dk. Mpango alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya uzinduzi wa mchakato wa maandalizi ya kuandaa Dira ya Taifa ya mwaka 2050, ambayo itatoa maono na malengo taifa linataka kuyafikia kwa kipindi cha miaka 25 ijayo.

Aidha, alisema pamoja na hatua kubwa iliyofikiwa nchi bado imeendelea kukabiliwa na kero mbalimbali zilizosababisha malengo ya dira ya 2025 kutofikiwa kwa ukamilifu.

"Kwa mfano tumeendelea kukabiliwa na changamoto ya umaskini wa kipato na lishe duni, takriban asilimia 26.4 ya Watanzania wote bado wanaishi chini ya kiwango cha umaskini wa kipato na maskini zaidi wanaishi vijijini ambao ni asilimia 31.3," alisema Dk. Mpango.

Vile vile, alisema bado kuna mikoa kama Kagera, Kigoma, Singida, Tabora na Dodoma ambayo kiwango cha umaskini ni kikubwa zaidi kwa sababu mbalimbali zikiwamo za kihistoria na miundombinu duni.

Kadhalika, alisema tofauti ya kipato miongoni mwa Watanzania imeendelea kuongezeka licha ya kufanya vizuri katika kigezo cha ukuaji wa uchumi.

Alisema kiwango cha tofauti ya kipato kwa kutumia kipimo cha uwiano kiliongezeka kutoka 0.34 mwaka 2011/12 hadi 0.38 mwaka 2017/18.

"Katika kipindi kama hicho, kipimo cha tofauti ya kipato katika maeneo ya mijini nacho kiliongezeka kutoka 0.37 hadi 0.41 na maeneo ya vijijini, kutoka 0.29 hadi 0.32.

"Utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria kwa mwaka 2022, unaonesha kuwa asilimia 30 ya watoto walio na umri chini ya miaka mitano wana udumavu na asilimia tisa ya watoto wana udumavu mkali," alisema.

Kuhusu kudumisha amani na usalama alisema Tanzania inajivunia kuwa kisiwa cha amani.

"Nchi yetu imeendelea kuwa na amani, utulivu, umoja, mshikamano na ni ya mfano katika Bara la Afrika. Hata hivyo, ni lazima tuendelee kuzilinda na kuzitunza tunu hizi katika kipindi cha miaka 25 ya Dira mpya kwa sababu bila amani, usalama na umoja hakuna maendeleo," alisema.

Dk. Mpango alisema kuhusu utawala bora nchi imepiga hatua kubwa katika kujenga na kuimarisha utawala wa sheria, haki na demokrasia na mhimili wa mahakama umeimarisha kazi ya kutoa haki kwa wananchi.

Alisema serikali kwa upande wake, inazingatia sheria, mila na desturi za Watanzania katika uendeshaji wa shughuli za kiserikali.

"Hali kadhalika, uhuru wa vyama vya siasa na vyombo vya habari umeimarika sana. Hata hivyo, katika eneo hili, pamoja na jitihada kubwa ambazo zinaendelea kufanywa, bado zipo changamoto za rushwa, uvujaji wa mapato ya serikali, wizi, matumizi yasiyo na tija ya rasirimali za umma kama inavyobainishwa kwenye taarifa za mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na upungufu katika eneo la haki jinai," alisisitiza Dk. Mpango.



Hata hivyo, alisema kwa kuzingatia baadhi ya kero ni vyema maandalizi ya Dira 2050 pamoja na mambo mengine izingatie kuimarisha uwezo wa uchumi uliojengwa hadi sasa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Dira ya 2025.

"Jambo la pili ni kutumia fursa ambazo hatujazitumia ipasavyo hadi sasa na kuzikamata fursa zinazochipukia. Kwa mfano katika kilimo, Tanzania ina fursa kubwa ya kuwa ghala la chakula katika Bara la Afrika au hata Mashariki ya Kati, tukilenga uzalishaji mkubwa wa mahindi, ngano, shayiri, soya, sukari, mafuta ya kupikia, korosho, matunda, mboga, na viungo," alisema.

Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, alisema kabla ya uwapo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 imesaidia kuboresha huduma mbalimbali za kijamii, kielimu na kiuchumi.

"Kabla ya uwapo wa dira hii ya taifa ya 2025 kitendo cha wanafunzi wa darasa la saba kumaliza shule na kukosa nafasi kujiunga na kidato cha kwanza lilikuwa jambo la kawaida katika vijiji vyetu, lakini hivi sasa hali imebadilika sana," alisema Nchemba.

## Samia apangua mabalozi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemhamisha kituo cha kazi aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Humphrey Polepole na kumpeleka nchini Cuba huku nafasi yake nchini humo ikiendelea kubaki wazi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Rais Samia pia amemteua Balozi Luteni Jenerali mstaafu, Yacoub Mohamed, kuiwakilisha Tanzania katika Falme za Kiarabu (UAE).

Kabla ya uteuzi huo, Balozi Mohamed alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Uturuki, ambaye nafasi yake inachukuliwa na aliyekuwa Konseli Mkuu, Dubai, Iddi Seif Bakari.

Aidha, taarifa hiyo ilisema kuwa tarehe ya uapisho wa mabalozi hao itatangazwa baadaye.

Polepole tangu alipoteuliwa Machi 14, mwaka 2022 ametumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja na siku 20.

Mwaka 2020 aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli, alimteua kuwa Mbunge katika nafasi 10 za Rais kutoka nafasi ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi tangu Desemba 13, mwaka 2016.



TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

### TAARIFA KWA UMMA

**MAKADIRIO YA KODI YA MAPATO KWA MWAKA 2023 NATAREHE ZA UWASILISHAJI RITANI NA MALIPO YA KODI MBALIMBALI KWA MWEZI APRILI 2023**

**Dar es Salaam, 03 Aprili, 2023:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imebaini uwepo wa baadhi ya ***Walipakodi ambao hawajawasilisha ritani au kufanyiwa makadirio ya Kodi ya Mapato kwa mwaka 2023***, na kulipa kodi stahiki kwa mujibu wa sheria. Walipakodi hawa, wanakumbushwa kufanya hivyo kwani tarehe ya mwisho ilipaswa kuwa tarehe 31 Machi, 2023. Mamlaka itafanya ufuatiliaji wa karibu na kuchukua hatua stahiki kwa walipakodi watakaobainika kuendelea kukiuka matakwa ya kisheria katika uwasilisha ritani, kufanyiwa makadirio na kulipa Kodi ya Mapato.

Sambamba na hilo, TRA inapenda kuwakumbusha walipakodi wote juu ya wajibu wao wa kisheria wa kuwasilisha ritani za kodi na kufanya malipo ya kodi husika kwa mwezi Aprili, 2023. Tarehe za mwisho za kuwasilisha ritani na kufanya malipo ya kodi mbalimbali zimeainishwa hapa chini:

**Jedwali: Tarehe za mwisho za kuwasilisha ritani na kulipa kodi mbalimbali:**

| Na. | Aina ya Ritani | Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha na kufanya malipo |
|---|---|---|
| 1 | Ritani ya kodi ya mapato yatokanayo na Ajira (PAYE) kwa kipindi cha mwezi Machi 2023 | Kabla au mnamo tarehe 7 Aprili 2023. |
| 2 | Ritani ya kodi ya zuio kwa kipindi cha mwezi Machi 2023 | Kabla au mnamo tarehe 7 Aprili 2023. |
| 3 | Ritani ya kodi ya uendelezaji ufundi stadi (SDL) kwa kipindi cha mwezi Machi 2023 | Kabla au mnamo tarehe 7 Aprili 2023. |
| 4 | Ritani ya kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kipindi cha mwezi Machi 2023 | Kabla au mnamo tarehe 20 Aprili 2023. |
| 6 | Ritani za Kodi nyinginezo | Kabla au mnamo tarehe tajwa. |

Mamlaka inawakumbusha walipakodi wote kuwasilisha ritani zao sahihi na kulipa kodi stahiki mapema ili kuepuka riba na adhabu ambazo zinaongeza gharama za ufanyaji biashara bila sababu. Walipakodi wote wanakumbushwa kuwa hakutakuwa na nyongeza ya muda wa kuwasilisha ritani za kodi na kufanya malipo yake, isipokuwa kwa kufuata utaratibu wa kisheria wa maombi uliowekwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizopo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

**Tovuti** : www.tra.go.tz
**Namba za Simu bila malipo** : 0800-110 016 au 0800-750 075 au 0800-780 078
**WhatsApp** : 0744 23 33 33
**Barua pepe** : huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

**TRA MAKAO MAKUU**

217353102

# Ndumbaro ataka ufanyike utafiti makosa uhujumu uchumi vigezo kwenye sheria

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amezungumzia makosa ya uhujumu uchumi akipendekeza utafiti zaidi ufanyike ili kuweka vigezo vya aina ya makosa hayo ndani ya sheria.

Pia, Chama Cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimependekeza Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, iwe divisheni ya makosa ya jinai.

Waziri Ndumbaro alitoa mapendekezo hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akitoa maoni ya wizara yake mbele ya Tume ya Kuboresha Mifumo ya Hakijinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Othman Chande.

"Twende tukafanye utafiti na kutoa mapendekezo kwenye makosa ya uhujumu uchumi. Yako mengi na ni makosa muhimu tunahitaji sana ili kulinda uchumi wa nchi yetu, lakini tukafanye utafiti zaidi kwenye eneo hilo ili kuangalia na kuweka vigezo vya makosa gani yanastahili kuingia kwenye orodha au jedwali la makosa ya uhujumu uchumi," alisema.

Alisema wizara yake imekuwa na mjadala mzuri na Tume ambao utazaa mapendekezo mazuri zaidi kutoka wizarani katika eneo hilo.

Waziri Ndumbaro aligusia pia muundo wa Taasisi za Haki jinai kama Polisi, Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (DPP), Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na Mhimili wa Mahakama, akipendekeza kuwa ziwe na jukwaa linaloweza kuwasadia kubadilishana taarifa.

Alisema lengo la jukwaa hilo liwe ni kuwaunganisha wadau wote kwenye mfumo huo ili waweze kupata na kutoa taarifa kwa wakati.

"Kwanza tunahitaji kuwa na platform (jukwaa), ambapo wote wanaotekeleza majukumu ya hakijinai wataweza kubadilishana taarifa mbalimbali zinazohusu haki jinai... ilivyo sasa kila taasisi inafanyakazi kwenye kiota chake. Tumependekeza mbele ya tume hii kwamba tuendelee kuwa na hivi viota vyetu, lakini tuwe na mfumo wa kubadilishana taarifa zinazohusiana na mfumo wa haki jinai," alisema.

Kadhalika, amependekeza sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 ipitiwe ili kuruhusu makosa yote ya jinai yawekwe sehemu moja.

"Yakiwa kwenye sheria moja itamsaidia hata mwananchi kuelewa na hata vyombo vya utekelezaji kuweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi," alisema.

Alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuunda Tume hiyo na kuteua wabobezi wa mifumo ya hakijinai kufanyakazi hiyo.

Pia, alisema wizara yake ambayo inagusa mfumo wote wa hakijinai imetoa mapendekezo mengi kwa kuwa inajua 'kiatu kinabana wapi.'

Wakili Dk. Frank Mchomvu, kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), alisema wamependekeza taasisi zote za hakijinai ziboreshwe, baadhi ya vifungu vya sheria vifutwe na vingine vifanyiwe mabadiliko.

Alisema wamependekeza kifungu cha 36 cha Sheria ya Makosa ya Kiuchumi na Uhalifu wa kupangwa kinachotoa mamlaka kwa DPP kuzuia dhamana kifutwe.

Kadhalika wamependekeza baadhi ya vifungu kwenye sheria ya utakatishaji fedha na sheria ya ugaidi, viboreshwe na vingine vifutwe.

"Mapendekezo yetu yamegusa sheria nyingi sana ikiwamo uhujumu uchumi. Tumependekeza pia ile mahakama inayohusu makosa ya rushwa na uhujumu uchumi ingelikuwa divisheni ya makosa ya jinai kwa ujumla," alisema.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja akizungumza wakati akifungua kikao cha Bodi ya maji Taifa, kilichoandaliwa na Bodi ya maji ya Bonde la Wami Ruvu, mjini Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA HAULE**


VisionFund | World Vision



JOIN A BOARD THAT IS CHANGING LIVES AND IMPACTING CHILDREN'S LIVES IN TANZANIA

Last year, the VisionFund network of microfinance institutions impacted the lives of 3.5 million children all over the world. We are looking for dynamic leaders who want to be part of this journey.

VisionFund International is the microfinance arm of World Vision, the largest Christian relief, development, and advocacy organization in the world. The VisionFund network serves over 1.1 million clients, and has a portfolio of over USD$400+ million.

Active in more than 28 countries, VisionFund provides financial empowerment to families across Asia, Africa, Latin America and Eastern Europe.

VisionFund Tanzania is seeking outstanding leaders with skills in Microfinance, Banking, Finance, Audit and Risk and Corporate Governance to join the Board of Directors on a voluntary basis. The Board provides leadership, offers strategic advice, and supports the Chief Executive in setting the standards of the company.

Candidates must be committed Christians, fluent in English and Swahili and willing to devote two to three days per quarter during each calendar year for a term of three years, which is renewable based on performance and availability. Service to the Board is not on payable terms but on voluntary basis.

Female candidates are strongly encouraged to apply.

Please send an application letter explaining why you would like to be part of the Board with your CV to Joseph Mwita through **joseph_mwita@wvi.org** by **30th April 2023.**

Successful candidates will be required to provide pastoral/priest and professional references.

For more information about VisionFund, visit www.visionfund.org


# Aliyepata ajali mwendokasi adaiwa kupoteza kumbukumbu

INATOKA UKURASA 2

singeweza kumudu kutunza familia hii kwa sababu nami nina yangu inanitegemea," alisisitiza Shaban.

Amewaomba wadau na wenye mapenzi mema walioguswa na tukio hilo kumchangia chochote kwa namba ya 0655025260 jina Shaban Milanzi.

**SHUKRANI KWA MOI**

Alisema kama hatamshukuru Mungu aliyemnusuru kaka yake na mauti na MOI waliohangaika na mgonjwa asiyefahamika hadi akapona atakuwa hajakata shauku yake ya kuzungumza na mwanahabari.

"Namshukuru Mungu na jopo la madaktari wa MOI, wauguzi wamefanya kazi muhimu ya kumhudumia mtu asiyejulikana 'unknown' ni moyo wa ajabu walionao watoa huduma za afya hawa. Namshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake kwa kuweka vifaa vya kisasa ambavyo vimesababisha ndugu yangu kupata matibabu na kupona."

Alimshukuru Mkurugenzi wa MOI, Dk. Recpicious Boniface kwa moyo aliouonyesha wa kuwajali nyakati zote wakiwa hawajajitokeza kumfahamu ndugu yao na hata baada ya kujitokeza.

**FIDIA KWA MGONJWA**

Shaban alisema moja ya mambo aliyofutilia kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ni fidia ya ndugu yake ambako alijibiwa kuwa, kesi ya ajali hiyo iko polisi, lakini pia inahusu watu wawili tofauti DART na gari ndogo lililosababisha ajali.

Alisema kesi ya msingi ya kudai fidia inapaswa kufunguliwa na Osam aliyepata ajali pindi atakapopona.

Alisema kwa sasa DART waliwafikisha hospitali majeruhi wote zaidi ya 30 na kwa Osam wamegharamia vipimo na matibabu mengine ya msingi.

"Uongozi wa MOI ulituambia wamelipia matibabu muhimu, hivyo kwa hiyo sisi tulilipa gharama za dawa za maumivu, chakula na neti za mgonjwa," alisema.

Mke wa Osam, Esha Mohamed, alimpigia simu kumtaarifu kuwa kaka yake hajarejea nyumbani na alihoji kama wana taarifa, lakini alisema walikuwa sawa isipokuwa alikuwa ameaga kuna sehemu angeenda.

Alisema mke wake alimpigia simu kumueleza kuwa kaka yake hajarudi, ikiwa ni siku ya nne, akiomba kumuulizia sehemu anazofanyia kazi.

"Nilienda kweli kumuulizia anakofanyia majukumu yake, lakini wakasema hawajamuona na kuahidi kumpa taarifa ikiwa watamuona, hadi ilipofika siku ya tano nilienda anakofanyia shughuli zake nikakuta wameweka kijiwe wakimzungumzia mbona haonekani," alisema.

Alisema lilitoka wazo na kumuulizia kwenye ajali ya mwendokasi ndipo jitihada za kumtafuta zilianza na kufanikiwa kumpata akiwa MOI.

Alisema walipofika Muhimbili walishauriana kuanzia MOI ambako walisikia habari mgonjwa alihamishiwa huo kupitia vyombo vya habari na kufanikiwa kumpata ndugu yake.

# Rasimu mitaala mipya, sera ya elimu yaiva

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema rasimu za mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo na Mitaala zimekamilika na wakati wowote zitatolewa kwa wadau ili waone kilichopendekezwa na kutoa maoni mengine ya mwisho.

Prof. Mkenda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha kuwapitisha wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo katika rasimu hizo.

Alisema lengo la kufanya mapitio na mabadiliko hayo ni kutekeleza ahadi aliyotoa Rais Samia Suluhu Hassan ya kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na mabadiliko ya mitaala, ili kuwezesha kutoa elimu ujuzi na pia kuwezesha sera na mitaala kuakisi mahitaji ya sasa na baadaye.

Alifafanua kuwa katika kutekeleza hilo serikali iliunda kamati mbili, ya Mapitio ya Sera na ya Mabadiliko ya Mitaala ambazo zilifanya kazi ya kukusanya maoni ambayo yalichambuliwa na wataalam na kupata rasimu.

"Kazi ya kwanza ya kamati hizi ilikuwa kukusanya maoni ya wananchi na baadaye yalifanyiwa uchambuzi na kuwezesha kupatikana kwa rasimu ya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo toleo la mwaka 2023 na Rasimu ya Mitaala mipya," alisema Prof. Mkenda.

Kadhalika, alisema wizara itafanya kongamano la siku tatu na itatoa rasimu hizo kwa wadau ili wapitie mapendezo na nafasi ya kutoa maoni kabla ya kufikia hatua ya mwisho.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo Prof. Kitila Mkumbo, aliishukuru wizara kwa kuona umuhimu wa kuipitisha kamati hiyo katika rasimu hizo ili nao waweze kutoa maoni yao.

Alisema kazi iliyofanyika ni kubwa ambayo inapaswa kupongezwa kwa kuwa kupatikana kwa toleo jipya la sera ya elimu kutawezesha wabunge kufanya kazi wakiwa na nyenzo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Husna Sekiboko, alisema maboresho yatakayofanyika yatainua ubora wa elimu na kuitaka wizara baada ya kuridhiwa utekelezaji wake uanze mara moja, huku akiitaka kuanza kutenga fedha katika bajeti za maandalizi ya utekelezaji huo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo, aliwaambia wajumbe wa kamati hiyo kuwa maboresho hayo hayataishia katika ngazi ya elimu msingi pekee, yatakwenda mpaka ngazi ya elimu ya juu.

# Taasisi ya kilimo yazindua kampeni 'Kijanisha Maisha'

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS Trust), imezindua kampeni ya Kijanisha Maisha na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo mkoani Singida kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji unaozingatia ukuaji wa kijani shirikishi.

Mkutano huo ulijadili njia za kuharakisha na kuimarisha maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa kutilia mkazo Ajenda ya Ukuaji wa Kijani Shirikishi kwa kilimo endelevu kitakachotosheleza mahitaji ya kujikimu, kibiashara na kuhakikisha usalama wa chakula cha uhakika na kilimo stahimilivu.

Kwa mujibu wa PASS Trust, usalama endelevu wa chakula utafikiwa kupitia mapinduzi ya kilimo yenye uthabiti na uendelevu kwa kuzingatia kanuni za Ukuaji wa Kijani Shirikishi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo katika mkutano huo, Meneja wa maendeleo ya biashara wa PASS Trust, Herman Bashiri, alisema ina mchango mkubwa katika kuchochea na kuwezesha ukuaji wa kilimo nchini huku kikitoa kipaumbele kwa vijana na wanawake kuwapa dhamana ya mikopo na huduma za maendeleo ya biashara ili kufikia malengo yao.

Alisema kuwa wakulima wananufaika na PASS Trust kwa kuwekewa dhamana ya mikopo ya kilimo, mifugo na uvuvi kupitia benki mbalimba nchini.

"Tunatoa dhamana ya hadi asilimia 80 ya mikopo kwa wakulima, wavuvi, wafugaji na wenye viwanda wanaozalisha kwa kufuata kanuni za uhifadhi wa mazingira na kupitia kampuni yetu tanzu ya PASS Leasing pia tunawezesha upatikanaji wa zana za kilimo," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alitoa pongezi kwa PASS Trust kuja na mpango wa Kukuza Uchumi kupitia ajenda ya Ukuaji wa Kijani Shirikishi, akisema ni njia bora ya kuchochea kilimo endelevu.

"Naipongeza PASS Trust kwa ubunifu na kuanzisha ajenda ya Ukuaji wa Kijani Shirikishi ambayo kwa hakika inachochea maendeleo endelevu ya kiuchumi ambayo yanaenda sambamba na utunzaji wa mazingira na kuongeza tija katika uzalishaji wa kilimo," alisema.

IITA Transforming African Agriculture — ILRI

## POSITION ANNOUNCEMENT
## RESEARCH ASSOCIATE 2 – DATA SYSTEMS
## IITA-TZ-2023 - R4D-005 -NRS-DSM

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Livestock Research Institute (ILRI) invites applications for the position of **Research Associate2 – Data Systems.** The Research Associate 2 – Data Systems will contribute to livestock production/productivity and genetic data management systems (collation, processing, and storage) and tools for use in the African Dairy Genetic Gain Project Country Program

**Duty Station: This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Dar es salaam - Tanzania.**

**Roles and Responsibilities:**

- Contribute to livestock production/productivity and genetic data management systems (collation, processing, and storage) and tools for use in the African Dairy Genetic Gain Project Country Program
- Understand existing tools used for data capture and assist in developing modules that extend the scope of the current tools and provide training for the same.
- Respond to ICT support requests from farmers, and field-based partner agents in a timely manner through WhatsApp/telegram/telephone/field visit programs.
- Write procedures and software to import/ export data from/to appropriate database systems and share these for further analyses and interpretation.
- Develop additional dashboards to enable monthly data monitoring of field agents submitting data per cluster, missing and incomplete information, unusual values, and other related issues and prepare a monthly report for the Country coordinator.
- Implement and monitor Quality Assurance (QA) protocols and routines, including safe and remote back-up of database systems and tools.
- Keep up to date with the latest tools and resources, including open-source software, for the collection, management, storage, and sharing of information.
- Maintain the confidentiality of all information collected.
- Participate actively in ADGG country meetings and workshops.
- Participate, plan, and facilitate training of partners on ADGG systems.
- Provide 1st and 2nd level support to partners using the different technological platforms offered by ADGG.
- Facilitate onboarding of new partners into ADGG platform and offer technical & user support.
- Partner engagement on new platform requirements.
- Perform any other activity as assigned by the national coordinator.

**Qualifications and Experience:**

- BA/BSc degree in Information Systems, Database Management, Computer Science, or related discipline.
- Experience working with integrated database systems preferably for research projects, including large-scale socioeconomic and/or biological surveys e.g., MySQL, MS SQL Server, or Oracle.
- Experience with database design, database management, and computer programming, and with the application of quality assurance standards and procedures.
- At least 4 years of relevant work experience in digital data systems.
- Advanced experience with SQL language for data extraction and management of databases.
- Knowledge and experience of Linux operating system.
- Experience in software programming.
- Understanding and experience of working in applied agricultural research preferred.

**Additional skills:**

- Fluency in Kiswahili and English is essential to communicate in writing and speaking.
- Ability to communicate effectively with different stakeholders.
- Ability to manage field teams and uphold the highest ethical standards by inspiring trust and treating all people with respect and personal integrity.
- Ability to work in a fast-paced environment with researchers, enumerators, and livestock value chain actors.
- Excellent interpersonal and relationship-building skills and ability to work collaboratively with people at all levels and from multiple disciplines and cultures in a respectful manner.
- Willingness to travel locally, regionally, and internationally.

**General information:**
The duration of contract for the position is three years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mabadiliko yajayo ya mifugo, uvuvi umma tujiandae kuneemeka nayo

**NI** habari njema, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inasema imejiwekea mikakati kadhaa ya kuleta mageuzi kwenye sekta za mifugo na uvuvi, ili kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa na maendeleo ya nchi.

Mikakati hiyo imekuja baada ya kugundua kuwa hali ya uzalishaji bidhaa hizo upo chini ya matarajio huku Waziri mwenye dhamana, Abdallah Ulega, akizungumza kupitia mtandao uitwao 'Club House' alitoa mfano samaki wanaozalishwa nchini ni wastani wa tani 350,000 kwa mwaka, huku mahitaji yakiwa tani 700,000.

Maboresho ya Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006 yanalenga kuvuka mazingira ya sasa, kwa kutoa mchango chanya katika maendeleo ya nchi, na kwamba imefikia hatua ya mwisho.

Mchango wa sekta hiyo kwenye pato la taifa uko chini, ikilinganishwa na sekta nyinginezo.

Licha ya kuwapo mifugo mingi nchini, lakini inachangia asilimia saba, ambayo mchanganuo wake ni ng'ombe milioni 80, mbuzi milioni 28, kondoo milioni 20 huku samaki wakichangia asilimia 1.8 ya pato la taifa.

Kwa maoni yetu mtazamo huo wa kiuzalishaji na utajiri wa kimiliki ya mazao hayo, mifugo ni tunu inayopaswa kugeuka katika sura ya utajiri wa nchi, hata sifa yake ikadondokea neema ya mtu mmoja mmoja. Tunatambua kwamba sio nchi zote barani Afrika zenye neema ya tunu hizo kama ilivyojaliwa nchi yetu, ambayo inaweza kuwa eneo litakalotoa ajira kwa wingi ikiwa litaendelezwa ipasavyo.

Haya yanajieleza unapotembelea kwenye fukwe au kunakofugwa samaki namna watu wengi wameajiriwa na kujiajiri, ndio maana tunaona kuna umuhimu wa kuimarisha sekta hizo ili mchango wake kwa taifa uzidi kuonekana.

Hiyo pekee kwa tuliopo kando tunaofuatilia, ni salamu njema zinazohitaji baraka zote kwa ajili ya kushuhudia utajiri kupitia sekta za mifugo na uvuvi.

Vilevile, salamu za waziri ni kwamba, wana mpango wa kuboresha upatikanaji majani na maji katika hali endelevu, wengi ikituachia ujumbe sasa ni safari mpya kuelekea kwenye ukingo wa simulizi za ugomvi, kati ya wakulima na wafugaji. Kwa upande wa uvuvi si haba, ni kwamba serikali inatoa fedha katika bajeti iliyopo sasa, Sh. bilioni 20 mahsusi kwa ajili ya kuboresha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria, lengo ni kukuza ubora wa bidhaa hiyo ili ikubalike sokoni.

Ni jambo jema nako katika kile kutoka kauli ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Riziki Shemdoe, anayesema mwaka huu serikali imenunua ng'ombe takribani 800 na kuwagawa kwa vikundi vya wafugaji madume bora katika halmashauri mbalimbali nchini, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa sekta hiyo.

Pia anataja kuwapo mashamba darasa 100 ya kuzalisha nyasi za kulisha mifugo lengo, hapo napo inatoa picha zaidi ya mikakati endelevu, wafugaji na wajasiriamali wanapewa darasa namna ya kuzalisha nyasi kwa ajili ya kulisha mifugo na kuuza.


Tunaamini kama mikakati hiyo ikitekelezwa ipasavyo, malengo ya wizara yatatimia na kuongeza soko la mifugo maradufu ndani na nje ya nchi, hata kuleta tabasamu na kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Pia, imani iko kwamba itaisaidia nchi kuzalisha nyama na samaki wa kutosha kwa Watanzania kula, hata kuwaepusha na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa protini ikiwamo udumavu.

Tunawasihi wadau wa samaki, nyama, vijana na wazee kushirikiana na serikali kukuza uzalishaji hadi soko, hata tukaona mapinduzi ya kiuchumi nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Unachotufanyia miradi hii Mwanza, Rais Samia unatuachia kumbukumbu

Na Anthony Gervas, MWANZA

**HEKO** Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kuwahakikishia wana Kanda ya Ziwa, miradi yao mikubwa ya kimkakati inakamilika kwa wakati,ikiwemo ujenzi wa daraja kubwa kuliko mengine Afrika Mashariki la JPM, Kigongo- Busisi.

Daraja hilo linatarajiwa kukamilika mnamo Februari mwaka 2024, litakalogharimu kiasi cha shilingi bilioni 716, hadi kukamilika ujenzi wake.

Macho na masikio ya wananchi wa Kanda ya Ziwa yameelekezwa katika miradi hiyo, ukiwamo wa ujenzi wa meli mpya ya kisasa ya 'MV. Hapa kazi Tu',ambayo imeshushwa majini kwa ajili ya kukamilisha hatua za mwisho za ujenzi huo.

Serikali ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan imewaondolea wasiwasi na hofu mioyoni mwao wananchi, wakipata matumaini makubwa ya kukamilika miradi hiyo, ambayo itawapa fursa nyingi kimaisha, zikiwamo ajira kwa vijana.

Hatua anazozichukua katika serikali yake ya awamu ya sita, zinadhihirisha kuwa utendaji kazi alio nao ni imara. Amethubutu kuhakikisha wasaidizi wake hawamuangushi kusimamia miradi ya kimaendeleo, katika kusukuma mbele uchumi wa taifa.

Hiyo ni ngazi moja, pia tuna daraja la JPM lenye urefu wa kilomita 3.2, nalo nasi tulioko tunamuona rais wetu, anavyotupigania kukamilika kwake, hata kufungua fursa nyingi kwa Kanda ya Ziwa, kiuchumi, kibiashara na kuongeza pato la taifa, kupitia huduma za kibiashara kutoka nchi jirani kama Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC) na Kenya.

Shabaha ya serikali hivi sasa, katika awamu ya sita ya uongozi wa nchi ni kuondoa minong'ono, mashaka na malalamiko ya wananchi, ambao walijawa wasiwasi au presha wakidhani miradi hiyo haitakamilika kujengwa.

Hivi sasa wanashuhudia uwezo uliopo katika kuwakomboa, rais mwanamke ukiwa mwanamama, unayeonyesha uwezo wa kusimamia kazi usiku na mchana, pasipo kutegemea kuwezeshwa.

Sote tunafahamu miradi hiyo ilianza kutekelezwa katika Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya hayati Rais Dk. John Magufuli mtangulizi wake, yeye akiwa Makamu wa Rais Dk.Samia amethubutu kuisimamia, kuendeleza ya mtangulizi wake na kuanzisha mingine mipya.

Akisimika kauli mbiu 'Kazi Iendelee',huku watanzania wengi wakishangilia kwamba anaupiga mwingi,haina ubishi kuwa anapambana vilivyo kuhakikisha Tanzania anaivusha kiuchumi na maendeleo pale ilipo sasa.

Binafsi nampongeza hata mimi,nampa heko za kauli mbiu yake 'kazi iendelee',sababu ni rais jasiri ambaye hawaonei aibu watendaji wadanganyifu,amekuwa akiwaonya,wengine kuwang'oa kabisa katika nafasi zao,wale wapigaji wa fedha za serikali za miradi ya maendeleo.

Mradi mwingine mkubwa ni ule wa ujenzi wa Meli mpya ya kisasa Mv"Hapa kazi tu,ambayo ni kubwa kuliko zote katika Ziwa Victoria, inayotarajiwa kukamilika agosti mwaka huu, itakayogharimu zaidi ya shilingi bilioni 100 kukamilika.

Haina longolongo bali Serikali yake inapambana kuhakikisha wananchi wanapata fursa za kutosha kupitia miradi hiyo,ikiwemo pia ujenzi wa bandari ya nchi kavu ya Fela wilayani Misungwi na reli ya kisasa (SGR) kutoka Mwanza hadi Isaka Kahama.

Ujenzi wa meli ya MV,Hapa kazi tu ni mradi ambao unasubiriwa pia kwa hamu kukamilika,wananchi wa kanda ya ziwa na taifa kwa ujumla,ili kufungua milango ya kiuchumi, kibiashara, kutoka nchi za Uganda na Kenya ambako itakuwa ikifanya safari zake kutokea bandari ya Mwanza.

Rais Dk.Samia ameweza kupanga safu ya viongozi wa juu wakiwamo mawaziri kwa umahiri, kama kwao kinamama wa katika orodha kamili, nao wakionyesha kupambana kuhakikisha nchi inasonga mbele zaidi kimaendeleo na uchumi.

Watendaji wake hao amewatia nguvu za ujasiri, pale wanapotoa uamuzi sahihi, wasitegemee maagizo yake, ili mradi watende haki wakati wa kuwahudumia Watazania.

Uthubutu wake unampandisha zaidi na kumpa heshima kubwa afrika na nje ya bara letu, akipata sifa ya kiongozi mahiri mwanamke anayeng'ara. Pasipo na shaka sasa amekuwa mfano.

Sasa anasonga akiwa mwamba wa siasa na demokrasia, akiwa marejeo kwa nchi za Afrika Mashariki kisiasa.

# Wananchi Mpanga wapewa angalizo mipaka ya hifadhi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMISHNA wa Uhifadhi Nyanda za Juu Kusini kutoka Mamlaka ya Wanyamapori (TAWA) Joas Makwati, amewataka wananchi wa Kijiji cha Mpanga, Kata ya Luduga, wilayani Wanging'ombe, Mkoa wa Njombe, kuheshimu mipaka ya hifadhi na kujiepusha kuingia ndani ya eneo la hifadhi kufanya shughuli zozote za matumizi ya ardhi kinyume na sheria.

Rai hiyo ilitolewa wakati wa kuweka mipaka katika Kijiji cha Mpanga kinachopakana na hifadhi ya pori la akiba Mpanga Kipengere kutokana na agizo la kamati ya mawaziri wanane wa kisekta la kushughulikia migogoro ya mipaka.

"Pori la akiba la Mpanga Kipengere lilianzishwa mwaka 2003 na lengo kuu ni uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji vinavyopatikana ndani ya hifadhi," alisema Makwati.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, serikali kupitia jopo la kamati ya mawaziri wanane limekuja na suluhisho la kutekeleza uamuzi wa serikali kuhusu hilo eneo kwa kuanza kuweka mipaka rasmi ili kuzuia wananchi wasifanye shughuli ndani ya hifadhi.

"Ekari 25,400 zimemegwa kwenye eneo la Hifadhi ya Mpanga Kipengere, kwa hiyo tunachoomba wananchi ni kuheshimu sheria, tutakapokuwa tumeweka mpaka tuheshimu sheria, watu wasiende kule ndani kufanya uharibifu, lakini watu wasiharibu mazingira kwa sababu yanatusaidia kwa ajili ya kupata mvua na mazao mengine," alisema.

Makwati alisema serikali kwa sasa ina mpango mkakati wa kuendeleza utalii Kusini mwa Tanzania, Hifadhi ya Mpanga Kipengere ni sehemu mojawapo ya mkakati wa serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kukuza utalii.

Mkuu wa Idara ya Ardhi, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Naili Mbyopya, aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kuheshimu maelekezo yaliyotolewa na kamati ya mawaziri wanane waliofika kwenye kijiji hicho Novemba, mwaka jana kutovamia kwenye pori la hifadhi hadi mipaka itakapowekwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Wanging'ombe Aginetha Mpangile aliishukuru serikali kwa kuanza kuchukua hatua za kutatua migogoro ya vijiji kwa kuwa uzinduzi huo wa mipaka utakuwa na suluhisho la kutatua migogoro.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, aliwakumbusha na kusisitiza wananchi wote kuendelea kuhifadhi vyanzo vya maji na kuepuka kufanya shughuli zozote za kibinadamu ndani ya hifadhi na kwamba serikali haitasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakaye kwamisha.

"Niungane na ninyi wananchi kumshukuru sana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na serikali kwa anavyoendelea kutatua kero na migogoro mbalimbali ikiwamo iliyokuwapo katika eneo hili la Mpanga Kipengere," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga (kulia), akisaini kitabu katika ofisi za Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Makumbusho Dar es Salaam juzi, alipofika kujadiliana na Mkurugenzi wa shirika hilo, Janeth Mawinza (kushoto), kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu haki za binadamu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Kuu yataka wadau kutumia TEHAMA

**Na Kulwa Mzee,** MOROGORO

MAHAKAMA ya Tanzania imewataka wadau wake kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili waweze kwenda pamoja katika kutekeleza majukumu.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Morogoro, Paul Ngwembe, alisema hayo jana wakati anafungua mafunzo ya siku nne kwa waandishi wa habari wa mahakama, wahariri wa habari na maofisa wa habari wa mahakama yaliyolenga kuwajengea uelewa wa kuripoti kwa usahihi habari za mahakama.

Jaji Paul aliwataja wadau wakuu wanaopaswa kuiga mfano wa mahakama kuwa ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na mawakili wa kujitegemea.

Alisema mifumo inayoitumia ya Tanzlii II, e Wakili, 'video conference', 'call center' na usajili kwa njia ya mtandao imesaidia katika shughuli za mahakama.

"Mahakama ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika matumizi ya Tehama kwa kuwa na mifumo mbalimbali inayowezesha utekelezaji wa majukumu yake.

"Mahakama ipo katika mapinduzi ya viwanda ambapo inataka inayoyatenda yawafikie wananchi ndani ya dakika chache bila ya kupotoshwa.

"Wito wangu kwa wadau wa mahakama wakuu ambao ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imegawanyika sehemu mbili Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na mawakili wa kujitegemea, waige mfano wa Mahakama matumizi ya Tehama katika shughuli zake twende pamoja," alisema Jaji Ngwembe.

Alifafanua kuwa mfumo wa Tanzil II unachapisha uamuzi, sheria na kuifanya Mahakama kutembelea watu duniani kwa asiliami 82.7 huku nchi ya pili inayofuatia kutembelea kupitia mfumo huo kuwa na asilimia 2.4.

"Kwenye Tanzlii kunaonyesha hukumu kwa uwazi na mashauri takriban 30 yanayoendelea duniani ni rafiki na haina gharama yoyote," alisema.

Jaji Ngwembe akizungumzia mfumo wa e Wakili, alisema unasaidia kupunguza mawakili vishoka kwa kuwa inaonyesha mawakili waliosajiliwa na picha zao na kupunguza uhalifu wa kisheria.

Pia, alisema mfumo wa e Wakili unawafanya wananchi kumtambua wakili aliyesajiliwa kwa kuingia katika mfumo ambapo atatambua yupi ni wakili," alisema.

Kuhusu mfumo wa video conference, alisema unasaidia usikilizwaji wa mashauri bila ya kufika mahakamani na unasaidia kupunguza gharama za wenye mashauri huku wa call center unasaidia mwananchi kupiga simu na kupata huduma popote alipo ndani ya saa 24.

Aliwaomba waandishi wa habari, wahariri na wananchi kutembelea mifumo hiyo kupata uamuzi mbalimbali uliofanyiwa kazi na iwapo kuna jambo wamelisikia wawasiliane na wahusika wapate taarifa.

Aliwaomba washiriki wa mafunzo hayo kutangaza maboresho yaliyofanywa na mahakama ikiwamo mifumo na jinsi Tanzania inavyoongoza Afrika kwa kuwa na majengo sita ya vituo jumuishi vya utoaji haki.

Mratibu wa mafunzo, Dk. Patricia Kisinda, alisema mafunzo hayo yameandaliwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# TEF: Mifuko hifadhi jamii chanzo kikubwa kukuza mitaji ya watu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF), limesema nchi zilizoendelea, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa chanzo kikubwa cha kukuza mitaji ya watu.

Vile vile, Jukwaa hilo limepongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kwa hatua yake ya uwekezaji wa ubia ambao umeonyesha ukomavu wa mfuko huo katika kukuza uchumi wa watu.

Mwenyekiti TEF, Deodatus Balile, alisema hayo wakati wa ziara ya wahariri wa kutoka vyombo mbalimbali vya habari katika kiwanda na Machinjio ya kisasa ya Nguru Hills, Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro.

"Uwekezaji hapa ni mkubwa sana, Serikali niwaombe PSSSF wahakikishe mradi huu wanaulinda na miradi mingine, sio vyema baada ya miaka kadhaa mbele ukija tena tuambiwe kilikuwepo kiwanda kisa wafanyakazi hawakutimiza wajibu wao vizuri," alisema Balile.

Awali, Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Eric Cormack alisema mradi huo una uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,500 kwa siku.

Alisema soko la nyama inayozalishwa kwenye machinjio hayo imepata soko la nje ya nchi kwa asilimia 80 zikiwamo za mashariki ya kati hasa Oman na asilimia 20 kwa ajili ya soko la ndani.

Alisema mahitaji ya nyama katika nchi hizo bado ni makubwa huku akitoa mfano mahitaji kwa nchi ya Saudi Arabia pekee kwa mwaka ni tani 700,000.

Cormack alisema, kwa nchi za kiarabu mahitaji ya nyama yataongezeka zaidi kufikia mwaka 2026 kwa tani 3,100,000.

Alisema mradi una miundombinu muhimu ikiwamo eneo la malisho lenye ukubwa hekta 2,328, kutunza ng'ombe 10,000 na mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja, na visima vitano vyenye uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa saa.

Alisema, usafirishaji wa nyama utaongezeka katika kipindi kifupi kijacho baada ya kupatikana kibali cha ISO kwa bidhaa za kiwanda hicho kutambulika kimataifa na hiyo itakuwa rahisi kuuza bidhaa zao kwenye mataifa mbalimbali duniani na hasa Saudi Arabia.




Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana wa Chama cha ACT- Wazalendo, Abdul Nondo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitoa pongezi kwa Naibu Katibu wa Chama hicho Bara, Joram Bashange kwa kushinda kesi inayohusu wagombea kupita bila kupingwa iliyokuwa imefunguliwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wanaosadikiwa majambazi waua mlinzi dukani, wapora fedha

**Na Samson Chacha,**

**TARIME**

MLINZI wa ghala la mchele katika kitongoji cha Forodhani, Kata ya Sirari Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime mkoani Mara, Juma Mwiri Chacha (38) ameuawa kwa kupondwa na jiwe kichwani na ubongo kutoka nje na watu wanaosadikiwa kuwa majambazi waliovunja maduka na kupora fedha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, mmiliki wa ghala hilo, Magwi Mangera alisema: "Niliondoka ghalani hapa jana jioni na kumwacha mlinzi wangu ambaye pia ni binamu yangu, Juma Chacha akiwa mzima nimepata taarifa alfajiri ya kuamkia Aprili 3, kutoka kwa watu waliopita asubuhi na kuona mwili wa mlinzi huyo ukiwa umetapakaa damu huku ukiwa pembeni mwa jengo hili la ghala.

Alisema mtu huyo alimpondda tena na kisha kumburuza kwenda pembeni mwa jengo na kuuacha mwili wake.

Alisema watu hao walivunja kufuli na kuingia ndani ya ghala na kupekua droo na sehemu nyingine kisha wakaondoka.

Mmiliki wa duka la vinywaji vya jumla, Matiko Rhimo alisema alipata taarifa za kuvunjwa kwa duka lao na kuibiwa fedha zaidi ya Sh. milioni 20 na walipofika walikuta umati wa watu huku mlinzi wa ghala la mchele akiwa ameuawa.

Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, ACP Geofrey Sarakikya, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo huku wakiendelea na uchunguzi.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Forodhani, Amon Mchuma, alisema kuna tatizo kubwa la kuongezeka kwa matukio ya uhalifu nchini.

# ATCL yajipanga kusafirisha mizigo mingi nje

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHIRIKA la Ndege nchini ATCL, limewahakikishia wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa upatikanaji wa huduma ya uhakika ya usafirishaji wa mizigo nje ya nchi, ikiwamo ya mazao ya mifugo na uvuvi yanayozalishwa kwa wingi katika mikoa hiyo baada ya serikali kununua ndege ya mizigo itakayoanza kutoa huduma baada ya kuwasili nchini hivi karibuni.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Mhandisi Ladslaus Matindi, mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wadau wa sekta ya anga na taasisi za umma kuhusu mategemeo ya shirika hilo kupata mizigo mingi kanda hiyo.

"Nia kubwa ya ujio wa ndege hii ya mizigo aina ya BOENG 767-300F ni kuhakikisha walengwa na wanufaika ni watanzania, ikiwa ni pamoja na wakazi wa kanda hii ya ziwa pamoja na mambo mengine tayari zao la samaki linaendelea kuhitajika nje na hii ndege itaendelea kuwasaidia kuondoa adha ya usafirishaji wa zao hili," alifafanua Matindi.

Aidha, aliwataka wananchi kuchangamkia fursa ya kilimo cha mboga, ufugaji pamoja na uvuvi kutokana na mazao hayo kuwa na soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima aliwataka watumishi wa umma kuwasaidia wananchi wanapohitaji huduma ya usafirishaji mizigo baada ya ndege hiyo kuwasili nchini kwa kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa vibali na kuwawezesha wananchi kutumia fursa zilizopo.

"Hii ndege itafanyakazi kwa ufanisi mkubwa endapo wazalishaji wataitikia kama wanavyoitikia kwa sasa katika safari za kawaida za ndege, hakuna ndege inayofika mkoani hapa bila kuwa imejaa," alisema.

Baadhi ya wafanyabishara na wasafirishaji wa mizigo kutoka Kanda ya Ziwa walisema ujio wa ndege hiyo utawaondolea adha ya kusafirisha mazao ya samaki kwa muda mrefu kwa njia ya magari yenye majokofu kuelekea mkoani Dar es Salaam.

"Hali ya kijiographia ya mikoa ya Kanda ya Ziwa ilikuwa ikitulazimu kuendesha magari yenye majokofu kusafirisha samaki na nyama kwa zaidi ya saa 18-20 barabarani hali iliyoshusha ubora wa mazao yetu wakati mwingine kutusababishia hasara," alisema John Chobo msafirishaji.

Hivi karibuni serikali ilitangaza kununua ndege kubwa ya mizigo BOENG 767-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54 za mizigo kwa awamu moja hatua itakayorahisisha shughuli za usafirishaji wa mizigo kutoka na kuingia nchini.



# Waliosimamishwa uongozi BAKWATA Kilindi warejeshwa

**Na Dege Masoli,** TANGA

SAKATA la kusimamishwa kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wilayani Kilindi, Shekhe Mdoe Mussa na Katibu wake, Juma Kidunda, limechukua sura mpya baada ya baraza hilo kuwarejesha na kuwasimamisha wajumbe wengine na kutoa maelekezo saba.

Taarifa iliyotolewa juzi kwa vyombo vya habari na BAKWATA na kusainiwa na Shekhe wa Mkoa wa Tanga, Jumaa Luwuchu, ilieleza kuwa baraza hilo ngazi ya mkoa imetengua uamuzi wa Baraza la Mashekhe la Wilaya ya Kilindi kwa kuwasimamisha viongozi hao.

Taarifa hiyo ilieleza uamuzi huo ulifikiwa baada ya BAKWATA mkoa kufanya kikao cha majadiliano na wilaya hiyo na kubaini kuwa mkutano uliowasimamisha viongozi hao haukuwa halali, hivyo kubatirisha maamuzi hayo.

Baada ya mahojiano na viongozi wa Wilaya ya Kilindi tulibaini kasoro mbalimbali ikiwamo kutokukamilika kwa akidi ya wajumbe waliohudhuria kikao na hawakuwa halali kwa mujibu wa katiba tumetengua uamuzi wote na kuwarejesha Katibu na Mwenyekiti wake madarakani," ilieleza barua hiyo.

Pamoja na kuwarejeshwa kwenye nafasi zao viongozi hao, baraza hilo pia limefuta uteuzi wa baadhi ya wajumbe akiwamo Katibu wa Wilaya, Shekhe Yahaya Kalamba na Hamis Mtali aliyekuwa Kaimu Katibu wa BAKWATA Wilaya kwa madai kuwa uteuzi wao umefanywa na kikao kisichokuwa na mamlaka.

Hata hivyo barua hiyo, ilitoa maelekezo kwa Shekhe wa Wilaya hiyo, kutojihusisha na shughuli za usuluhishi na majukumu hayo yatafanywa na Kadhi wa Wilaya hiyo, Shekhe Waziri Mkwayu.

Pia ilimuagiza Mwenyekiti wa baraza hilo wilaya kuacha kufanya kazi za katibu.

Vilivile Baraza la Mkoa huo, liliahidi kufuatilia kwa karibu mienendo na utendaji wa viongozi hao na endapo watabaini wanakwenda kinyume na maelekezo hayo litachukuliwa hatua kali za kimaadili dhidi yao ili kuondoa migogoro ndani ya baraza hilo.

Aidha, umewataka viongozi hao kufungua ofisi ya wilaya na kufanyakazi siku zote, wakimuagiza Kadhi kutoa huduma kwa jamii pamoja na kuhakikisha anapata hati za kufungisha ndoa sambamba na kitabu cha ndoa.

**Pia ilimuagiza Mwenyekiti wa baraza hilo wilaya kuacha kufanya kazi za katibu.**

# Meya awaonya watoto wa mitaani kulala makaburini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iraqhe, ametoa onyo kali kwa watoto wa mtaani ambao wamegeuza makaburi kuwa sehemu yao ya kulala, kufanya mambo mengine ambayo hayapendezi katika jamii.

Alisema halmashauri ya Jiji hilo litaendesha kampeni ya kusafisha makaburi yaliyoko katika eneo hilo kwa ajili ya kuyaweka katika hali ya usafi wakati wote.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki aliposhiriki shughuli ya usafishaji wa makaburi yaliyoko Kata ya Levolosi mkabala na Kituo Kikuu cha Mabasi Mkoa wa Arusha.

**Wana wajibu wa kuonya kwa kuielezea jamii umuhimu wa kuielewa historia ya nchi ilikotoka ili kujenga uzalendo.**

"Natoa onyo kwa baadhi ya watoto wakiwemo wale wanaoishi kwenye mazingira magumu na hatarishi ambao wamegeuza makaburi kama ni sehemu ya kuishi, kulala, kupimzika, kuvutia bangi, kuwasha moto juu ya makaburi kwa kisingizio cha kuota moto kutokana na baridi,"alisema.

Alisema usafi huo utakuwa ukifanyika kila wiki kwa lengo la kuhakikisha makaburi yote ya Jiji la Arusha yanakuwa safi pamoja na makaburi mengine yakiwano ya Baniani.

Iraqhe alisema nchi zilizoendelea makaburi yaliyoko katikati ya miji huwa yanakuwa ni makumbusho, hivyo aliwaomba wananchi kuwa wazalendo kwa kushiriki kuyasafisha.

Katibu wa Umoja wa Wazee mkoani Arusha (UWAJIA), Salum Msuya, alisema wana wajibu wa kuonya kwa kuielezea jamii umuhimu wa kuielewa historia ya nchi ilikotoka ili kujenga uzalendo.

Kadhalika walieleza kuchukizwa na tabia za baadhi ya watu wanaotupa taka kwenye maeneo ya makaburi jambo ambalo siyo sahihi kwa kuwa maeneo hayo siyo jalala.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Kiria Laizer (wa pili kushoto), akimsikiliza Mkuu wa kituo cha polisi Mirerani, SP Dominick Fwaja, wakati akifafanua jambo kuhusu masuala ya ulinzi shirikishi na polisi jamii, walipokutana juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ofisa Madini amaliza mgogoro wa kugombea mgodi wa tanzanite

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

OFISA Madini Mkazi wa Mirerani, Mernad Msengi amemaliza mgogoro wa kugombea mgodi wa madini ya tanzanite, kati ya kampuni ya Njake Enterprises na Patrick Miroshi, ulioko katika Mamlaka ya Mji mdogo wa Simanjiro mkoani Manyara.

Mgogoro huo umefikia tamati juzi baada ya ofisa huyo wa madini kuonyesha mgodi huo ni mali ya kampuni ya Njake na eneo lenye mgogoro liko ndani ya lesini ya Njake.

Msengi alisema kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Madini, mgodi huo upo kwenye leseni namba PML 00416SMN ya Japhet Lema inayomilikiwa na Kampuni ya Njake Enterprises.

"Wahusika wa pande zote mbili walifika eneo hilo na kukubaliana upimaji ulivyofanyika kupitia vifaa vya kitaalam zaidi vyenye ufanisi tofauti na vifaa vya GPS ya kawaida," alisema.

Hata hivyo alisema kwa upande wa mipaka ya Patrick Miroshi, vipimo vimeonyesha kuwa mgodi huo upo nje ya eneo la umiliki wake kwa umbali wa mita 1.9 kulingana na mipaka ya leseni ya awali.

Aidha, alisema wamependekeza kuwa wachimbaji hao, Miroshi na Njake wachimbe katika mipaka ya leseni zao na siyo vinginevyo ili kuepusha na kumaliza migogoro inayojitokeza.

"Pande zote zizingatie sheria, kanuni na utaratibu wa uchimbaji madini na eneo tengefu ili kuwepo uchimbaji wa tija kwa maendeleo ya sekta ya madini na taifa kwa ujumla," alisema.

Meneja wa mmiliki wa awali wa mgodi huo, Mangoshi Seleman, ambaye aliuuza mgodi huo kwa Njake enterprises, Mohamed Mughanja, alisema uamuzi huo umetenda haki.

"Sisi tuliiuzia mgodi huu kwa Kampuni ya Njake Enterprises, lakini jirani yetu Miroshi akawa analalamika kuwa amedhulumiwa mgodi jambo ambalo siyo kweli na Wizara ya Masini imetoa majibu mazuri," alisema Mughanja.

Meneja wa Kampuni ya Njake Enterprises, Hassan Salehe, alisema wameridhika na uamuzi huo, kwa kuwa kabla ya kununua mgodi huo walifanya uchunguzi.

Hata hivyo, uongozi wa mgodi wa Miroshi ulisema haujaridhika na uamuzi ho, kwamba watatafuta wataalam huru wenye vifaa stahiki ili kurudia upimaji huo.



# Wanawake watoa vifaa tiba kusaidia watoto njiti

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIKUNDI cha wanawake mkoani Shinyanga kiitwacho Women For Change, kimetoa msaada wa mashine mbili kwa ajili ya kusaidia watoto wanaozaliwa kabla ya wakati ili kuokoa maisha yao.

Akikabidhi mashine hizo juzi kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Luzila John, Mwenyekiti msaidizi wa kikundi hicho, Lucy Mwita, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuokoa maisha ya watoto hao.

**Kikundi chetu tumekuwa tukishirikiana na serikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu kwa kununua madawati.**

"Kikundi chetu tumekuwa tukishirikiana na serikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu kwa kununua madawati, kukarabati mabweni na leo tupo upande wa sekta ya afya tumenunua mashine mbili zenye thamani ya Sh.milioni 24 ili kuokoa maisha ya watoto," alisema Lucy.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Luzila John, alisema mashine hizo zitakuwa msaada mkubwa katika kuongeza nguvu za kuokoa maisha ya watoto hao ambao wamekuwa wakipata shida katika upumuaji kutokana na kuzaliwa kabla ya muda na mapafu yao yanakuwa bado hayajakomaa.

Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Yustina Tizeba, alisema wamekuwa wakipata idadi ya watoto wengi ambao wanazaliwa kabla ya muda, hivyo kupata mashine hizo ni msaada mkubwa katika kuokoa maisha yao.




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (katikati), akikabidhiwa zawadi na Meneja Maendeleo ya Biashara wa Taasisi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS Trust), Helman Bashiri (kulia), wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Kijanisha Maisha kwa wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo, mkoani humo. Kushoto ni Meneja wa PASS Trust Kanda ya Masharikí na Kati, Hadija Seif. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ukosefu hospitali chanzo wajawazito kufariki

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

UKOSEFU wa kituo cha afya katika Kata ya Mwamalasa Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga limedaiwa kuwa chanzo kwa wajawazito katika kata hiyo kufariki dunia wakati wakijifungua.

Wakazi wa wilaya hiyo hulazimika kusafiri kilometa 70 kwenda Hospitali ya Dk. Jakaya Mrisho Kikwete kufuata huduma.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na wananchi wa kata hiyo wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga ya kukagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho katika kijiji na Kata ya Mwanamalasa.

Walieleza kuwa hali hiyo imekuwa ikiwasababishia adha kubwa hususani kwa wajawazito na watoto wadogo wenye umri chini ya miaka mitano.

Mbuke Bulugu alisema mwaka jana katika kata hiyo wajawazito watano walipoteza maisha kutokana na kukosa usafiri na kulazimika kujifungulia kwa wakunga wa jadi ambao wengi wao hawana utaalamu wa masuala ya uzazi.

Alisema nyakati za usiku wanapopata mgonjwa hasa mjamzito wanalazimika kutozwa Sh.300,000 hadi 400,000 na wamiliki wa magari binafsi ili kusafirisha mgonjwa kwenda hospitalini.

Alisema kwa wananchi wasio na uwezo wanalazimika kujifungulia kwa waganga wa jadi wasiokuwa na taaluma.

Mkazi mwingine, Moryanda Maziku alisema vijana wengi waliopo kwenye ndoa wamelazimika kununua basikeli au pikipiki kwa ajili ya kusafisha wagonjwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu, Emmanuel Johnsohn alikili kuwapo kwa tatizo hilo na kusema wametenga Sh. milioni 500 kutoka mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya na kuwaondolea adha hiyo.

"Kituo hiki kitakapokamilika tutahakikisha tunaleta watalaamu wa kutosha ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma stahiki ikiwemo za afya ya uzazi, kata hii ina wakazi 26,000 na wengi ni wakulima na wafugaji bila kusogezewa huduma za afya karibu watakimbilia kwa waganga wa jadi kupata huduma"alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mdeme aliwataka wananchi hao kutokuwa na wasiwasi kwani serikali imejikita kutatua kero mbalimbali za wananchi hususani katika sekta ya afya na elimu na kuahidi kuchangia mifuko 50 ya saruji ili kufanikisha ujenzi huo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlowa aliziagiza Wakala wa Usambazaji Maji Vijiji (RUWASA)na Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO) kuanza taratibu za kupeleka huduma ya maji na umeme katika kituo hicho ili pindi kinapokamilika wananchi waanze kupata huduma.

## Shule za sekondari zapewa msaada vifaa TEHAMA

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TAASISI ya Vodacom imetoa msaada wa vifaa vya TEHAMA vya Sh. milioni 150 kwa shule za sekondari 20 mkoani Tabora ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa uunganishaji wa shule.

Vodacom wanashirikiana na Taasisi ya African Child Projects na Mfuko wa Mawasiliono Sawa kwa Wote (UCSAF) ambao unalenga kuzifikia shule 300 nchini.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk.Batilda Buriani alipongeza jitihada za mpango wa uunganishwaji wa shule katika kuboresha mfumo wa ufundishaji na kujifunzia kuhamia kwenye mfumo wa kidijitali.

Meneja Mauzo Mwandamizi wa Kanda ya Ziwa, Ahmed Akbarali alisisitiza kuwa msaada wa vifaa vya TEHAMA ni sehemu ya utekelezaji wa adhma ya kampuni katika kuboresha maisha ya jamii za Watanzania kupitia ubunifu wa huduma na bidhaa za kidijitali kwenye sekta tofauti nchini kote.

Aliongeza kuwa katika awamu hiyo baadhi ya shule zitaunganishwa na huduma ya intaneti ya Vodacom Tanzania kwa mwaka mzima bila ya malipo, kwamba itawasaidia kupata maudhui bure kupitia jukwaa linalotoa elimu kidijitali la e-fahamu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kariakoo, Leonard Nyasebwa, alisema vifaa hivyo vitawasaidia katika kufundishia na kujifunzia pia itainua kiwango cha elimu katika shule hizo za sekondari.

Alisema: "Ni muda muafaka sasa kuanza kuzingatia uwekezaji kwenye miundombinu ya TEHAMA katika shule zote nchini. Kwa sababu ukiwa na miundombinu ya kiteknolojia huduma ya kufundishia na kujisomea mtandaoni itaweza kuwafikia kwa urahisi na haraka walimu na wanafunzi".



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk Batilda Buriani (katikati) akishuhudia makabidhiano ya msaada wa mojawapo ya kompyuta na vifaa vingine vya TEHAMA kutoka kwa Meneja Mauzo Mwandamizi wa Vodacom Tanzania Kanda ya Ziwa, Ahmed Akbarali (kushoto) kwenda kwa Mkurugenzi wa Youth Relief Foundation, Joachim William (kulia), ikiwa ni sehemu ya mradi wa uunganishwaji wa shule za sekondari unaolenga kuziunganisha shule 300 Tanzania.

Nipashe
# TESA
Jumanne APRILI 4, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12

Wadau elimu wazidi kushangilia katazo bweni, ushauri wao kulala shule kuanzie sekondari


Ukurasa 13

Waraka Namba 6; uamuzi ukitumika vyema, muarobaini endelevu dhidi ya matusi mtihani


Ukurasa 14

USHINDANI WA SHULE BORA KWENYE MIKOA TISA ...
Mradi unaotakatisha wanafunzi chekechea hadi kidato cha sita

TEKNOLOJIA

NA MARY GEOFFREY

# Kifuu kilivyo mbadala wa zebaki migodi ya dhahabu

•Ni dawa kusafisha madini,majitaka; mbunifu ataka Mil. 36 kumaliza shida

NI tunda lenye mamia ya faida, ukianza na kulitafuna kama chakula, ni kiungo hunogesha vyakula, machicha kulisha mifugo, ni kipodozi kwenye ngozi na nywele, pia huchanganywa na viambato vingine kutengeneza dawa.

Makumbi yanasukwa kupata kamba, makuti huezeka makazi na maeneo ya burudani, huku vifuu vikibadilishwa kuwa urembo na mapambo, mti wake ni mbao na hata kuni pia, hiyo ndiyo Nazi.

Ukikiangalia kifuu pekee kuna matumizi yenye faida tele kama kutengeneza vyombo mfano upawa, vijiko na bakuli, vyungu vya kupandia maua yote hayo hupendezesha nyumba na kuongeza kipato kama bidhaa zikiuzwa.

Mtafiti na mbunifu wa teknolojia ya kuzalisha hewa ukaa au kabon, Tiberius Mario, anasema kifuu ni fursa kubwa ya kiuchumi akitaja, kutengeneza kabon inayotumika kuchenjulia (kusafisha) madini na maji.

Akizungumza kwenye semina ya wanahabari inayoandaliwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Jijini Dar es Salaam, Mario anaeleza namna anavyotumia vifuu kubuni biashara inayomwingizia kipato, anayoifanya pia kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwa vile vifuu vinaweza kuwa mazalia ya mbu wanaoleta malaria.

"Nimebobea kutengeneza kabon au mkaa unaotumika kuchenjua dhahabu kusafisha maji taka, ninabadilisha kifuu cha nazi kwenda kwenye kabon ambayo kwenye


Kabon au mkaa unaotengenezwa na vifuu unaosafisha dhahabu. **PICHA: MTANDAO**

migodi yote Tanzania hauwezi kupata dhahabu bila ya kuwa na gesi hii baada ya kusafishwa dhahabu lazima ipitishwe kwenye kaboni ili dhahabu zitoke kwenye udongo,"

Anasema hakuna kiwanda cha kuzalisha mkaa huo na kwamba zinazotumika zinatoka nje akiongeza kuwa mikoa ya pwani na kusini inazo nazi nyingi zaidi ya tani 350,000 kwa mwaka na huzalisha vifuu vingi.

Baada ya kuviona vinazagaa kwenye majalala na havina kazi, anaibua fursa ya kutengeneza kabon na kwamba alianza biashara hiyo kwa kukusanya vifuu mwenyewe katika maeneo mbalimbali.

"Nilifanya utafiti wa kuzalisha, kidogo sasa nazalisha kwa wastani nilishapeleka kwenye baadhi ya migodi na viwanda vya maji, Inatumika kusafisha maji kwa kupunguza chlorine kwenye maji na kuondoa harufu," anafafanua

"Indonesia inaongoza kwa kuzalisha nazi, pia India na Tanzania ni namba 16 ambako inazalisha tani 382,164 kwa mwaka kiasi ambacho kinaweza kuzalisha vifuu vingi. Kwa kuangalia wingi huo naona fursa kubwa ya kutimiza ubunifu na kufikia malengo ya kumiliki kiwanda." Anasema Mario.

Mtafiti huyo anasema takribani tani 1,500 za mkaa inayotumika nchini huagizwa nje ya zikigharimu dola Milioni 6.7 karibu Shilingi bilioni 16.1 na kwamba kabon hiyo inaweza kupimwa katika maabara na utendaji wake ni asilimia 98 katika madini na maji pia.

"Nilipeleka Mbeya, Shelui na STAMICO na nilifikisha sampuli Tume ya Madini, matokeo yaliyotoka ni mazuri imekamata dhahabu kwa kiwango kikubwa

Pia ninaweza kuirudisha tena kwenye mfumo kabon ambayo inatumika kwa sababu ikitumika haitakiwi kutupwa ila zinahifadhiwa ili kuondoa mlundikano hivyo narudisha kwa kurejeleza".

**VIKWAZO**

Anataja mtaji na kwamba anachozalisha ni kilo 100, huku kiwango cha uhitaji kikiwa kikubwa zaidi, anatumia makaa ya mawe kama chanzo cha joto na kuni pia, kitaalamu anahitaji joto zaidi ya nyuzi 300,000 lakini kuni zinatoa joto la nyuzi 4,000 kwa kilo moja ili kupata nyuzi 300,000 anatumia kuni nyingi na muda mrefu.

"Nikipata Diesel Burn, joto lake ni kubwa ikilinganishwa na kuni na kifaa kinachotumika kutengeneza na kutoa bidhaa ninayotoa mimi ifike hata asilimia 90 sasa ni asilimi 50 nikiwezeshwa ninaweza kuchukua vifuu vyote na kutengeneza kabon na hatutaagiza nje nahitaji Shilingi Milioni 36,"anaeleza.

Anasema mfuko wa Kabon wa kilo 25, huuzwa Shilingi 250,000 hadi 400,000 inategemeana na nchi inakotoka ila kwa China wanauza kati ya Sh 250,000 na 280,000 na Amerika ni Sh 400,000 lakini rejareja kilo moja ni 20,000 hadi 25,000." Anasema Mario.

"Ni kitu cha gharama inaweza kuhitaji hata kilo 500 lakini uwezo wangu ni mdogo nikipata mtaji nitafanya vizuri, sio Nazi peke yake hata Mchikichi naweza kuutumia," anasema mbunifu huyo.

Mratibu wa Mafunzo ya Uandishi wa Habari za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kutoka COSTECH, Deusdedith Leoanaed, anasema lengo la kuwakutanisha wanahabari na watafiti ni kupata ongezeko la uhasilishaji wa teknolojia kati ya watafiti na jamii kuwajengea uwezo wanahabari ili waweze kuandika taarifa hizo kama ilivyo katika maeneo mengine ikiwamo siasa na michezo.

**AJIRA MADINI**

Takwimu zinaonyesha kuwa sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini inatoa ajira za moja kwa moja kwa zaidi ya watu milioni 1.2 na kwamba ajira zisizo za moja kwa moja zinawahusu watu milioni 7.2 ikiwa ni sawa na asilimia 13 ya idadi ya Watanzania.

Tathmini hiyo inaonyesha kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu hutumia tani 13.2 na 24.4 za zebaki kwa mwaka kusafisha madini hayo na kwamba kemikali hiyo ni sumu na kitisho kwa afya na mazingira.

Shirika la Afya Duniani (WHO),linaeleza kuwa ukitumiwa bila kuzingatia utaalamu huharibu ubongo na mfumo wa mishipa ya fahamu, figo, husababisha watoto wenye ulemavu, kupoteza kumbukumbu ikiwamo kushindwa kupumua.

Mbadala wa kemikali hiyo ni karbon kwa sababu ni salama zaidi ikilinganishwa na hiyo zebaki ambayo inaingizwa nchini kwa kificho huku watumiaji wakubwa

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA JALIWASON JASSON, BABATI

# Wadau elimu wazidi kushangilia katazo bweni, ushauri wao kulala shule kuanzie sekondari



Wanafunzi wa umri mdogo wakiwa bwenini. **PICHA: MTANDAO**

Wanaoagiza watoto wasikae bweni mpaka darasa la saba isipokuwa wakienda kidato cha kwanza ndio waruhusiwe ushauri unapokelewa na wadau wa elimu kwa udhati.

Kuanzia walimu, wazazi, walezi na asasi za kiraia kunaibuka, mitizamo chanya inayokubali agizo hilo mfano, Meneja Mkazi wa Shirika la So They Can Tanzania (STC) Roselyne Mariki, anasema wanafanya kazi na shule za msingi 28 za halmashauri ya wilaya ya Babati mkoani Manyara zenye watoto zaidi ya 17,000.

Anaongeza kuwa kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto ambao wanausikia kwenye vyombo vya habari.

Roselyne anaeleza kuwa malezi ya mtoto yanaanzia nyumbani anapopata msingi hivyo serikali kuja na waraka huu ni sahihi ili waendelee kulindwa na kutunzwa.

Anasema msingi wa malezi ya mtoto ni ngazi ya familia hivyo hawana budi kutekeleza waraka huo, anaongeza Grace Swai kutoka So they Can akiunga mkono waraka huo namba 2 wa elimu.

"Hawa watoto wa awali hadi darasa la nne wanahitaji uangalizi wa karibu kutoka kwa wazazi na walezi,"anasema na kuongeza kuwa watoto ni wadogo wanakumbana na ukatili na hawawezi kusema maana wanatishiwa wakiwa bweni.

Anapendekeza waraka ungesema watoto wasiishi bweni mpaka wakienda sekondari .

Aidha, anasema wakiachwa kuendelea kuishi bweni maadili yatazidi kuporomoka na kutakuwa na kizazi cha ajabu kisichoelezeka.

Nipashe inazungumza na Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Mji wa Babati Simon Mumbee anayesema waraka huo wameupokea na kwamba umri wa mwanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la nne unahitaji ukaribu wa wazazi.

"Unapowatoa nyumbani na kwenda kuishi bweni unawaathiri kisaikolojia na makuzi yao yatakosa maadili ya wazazi,"anaeleza Mumbee

Ofisa huyo anasema anaona bora wangefika darasa la tano ili wawe wanajielewa kidogo.

"Waraka umetoa muda hadi Juni mwaka huu wazazi watakuwa wamejipanga vizuri na utekelezaji wa sera hiyo anasema unaanzia Julai mwaka huu ndio wataanza kufanya ufuatiliaji kuona utekelezaji wake na kuona watakaokaidi huku akisema waraka huu umeletwa wakati sahihi.

Mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Kiongozi, Cesilia Sagara, anasema asilimia kubwa tabia na mienendo inabadilika kulingana na teknolojia na kwamba

malezi yarudishwe kwa wazazi na walezi ili kupunguza ukatili au kuumaliza.

Mshauri wa awali wa malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC) Davis Gisuka, anasema anaunga mkono waraka huo , akihoji

"Unampelekaje mtoto mdogo wa awali au darasa la kwanza akaishi bweni wakati ndio wa kujenga mahusiano ya karibu na familia, mlezi na mzazi?"

Anasema miaka 0 mpaka miaka nane mtoto anatakiwa akae na wazazi au walezi wake kwa kuwa hicho kipindi ni cha kujenga tabia ya mtoto.

Mtaalamu huyo wa malezi na makuzi anasema ndiyo wakati wa kujenga raia mwema au kuandaa wahalifu ni wakati huo huo.

Anayataja madhara yanayoweza kumpata mtoto anayeishi bweni akiwa na umri huo kuwa ni kukosa malezi ya wazazi, kuua mahusiano ya mzazi na mtoto hata akikua hawezi kuwa na muda na mzazi, chakula anachokula hakimtoshi na hakiwezi kufanana na cha nyumbani.

Anaeleza kuwa matokeo yake akikosa chakula bora atapata udumavu wa akili, wa ubongo na kisaikolojia itamwathiri.

"Hili jambo nilikuwa nalipigia kelele miaka mingi serikali imesikia kilio changu nashauri watoto waende bweni kidato cha kwanza,"anasisitiza

Bingwa huyo wa malezi na makuzi ya mtoto anasema watoto wanatoka mazingira tofauti kwahiyo kuna tabia ambazo hazifai na ndicho kipindi wanajifunza mambo mengi na ubongo unapokea.

Gisuka anasema katika umri wa miaka 0 mpaka miaka nane ubongo unashika vitu vingi haraka na kukaa kikamilifu kichwani kwa mtoto.

Kuhusu muda waliopewa Gisuka anasema angeombwa ushauri angeshauri serikali, isitoe muda huo badala yake utekelezaji ungeanza haraka.

Mkazi wa Mtaa wa Block X Musa Rehani(74) anasema waraka huo umechelewa kutolewa na serikali kwa kuwa ameupigia kelele miaka 20 iliyopita bila mafanikio.

Anasema mtoto wa darasa la kwanza na la pili anaendaje kuishi bweni na mapenzi ya mzazi atayapata wapi?

Anasema enzi zake alianza darasa la kwanza akiwa na miaka 13 na alisoma na wenzake wakiwa darasa hilo wananyoa ndevu na hayakuwepo mambo ya kupelekwa bweni.

Mzee huyo maarufu anasema watoto wa siku hizi wanakaa mazingira ya ajabu na kwamba mlezi au Patroni usiku ukiingia anaenda kulala wao wanabaki bweni wanaendelea na mambo yao ya ajabu.

"Utitiri wa shule za msingi binafsi zimechangia mmomonyoko wa maadili mtoto anajua ndiyo maisha akifanyiwa ukatili hawezi kuripoti mahali popote,"anasema Rehani.

Anafafanua kuwa mtoto akiachwa bweni anashindwa kujua kufanya kazi hata kufua nguo zake za ndani atashindwa.

Ikumbukwe kuwa Februari 28 mwaka huu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa waraka namba 2 kuagiza kuondolewa huduma za shule za bweni za wanafunzi wa awali hadi darasa la nne.

# KIFUU KILIVYO MBADALA WA ZEBAKI MIGODI YA DHAHABU

INATOKA UK.11

ambao ni wachimbaji wadogo wakiiitumia bila kufuata taratibu za ulinzi wa afya na mazingira.

Kwenye Mpangokazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu kwa mwaka 2020-2025 ambao umeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, inaelezwa kuwa tani 24 za kemikali hatari ya zebaki hutumika kwa mwaka katika shughuli za uchenjuaji wa dhahabu unaofanywa na wachimbaji wadogo.

Mpango Kazi huo, umekuja baada ya Jumuiya ya Kimataifa wa mwaka 2013 kupitisha Mkataba wa Minamata, wenye madhumuni ya kulinda afya ya binadamu dhidi ya madhara ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na zebaki, ambao Tanzania iliusaini mwaka 2020.

ELIMU

NA BEATRICE MOSES

# Waraka Namba 6; uamuzi ukitumika vyema, muarobaini endelevu dhidi ya matusi mtihani




Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa. **PICHA: MTANDAO.**

SERIKALI imetoa Waraka wa Elimu Namba Sita wa Mwaka 2022, unaohimiza Usimamizi wa Maadili kwa Wanafunzi wa Shule zote. Kimantiki unatajwa kwamba, unaweza kuwa muarobaini kukomesha majibu ya lugha chafu kwenye mitihani ya taifa na mingineyo kwa ujumla.

Waraka huo ulitolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia nchini Oktoba mwaka jana, ukiwekewa mkazo kwa shule zote kuwa na usimamizi makini, pia kutoa ushirikiano kati ya walimu na wazazi au walezi kwa ujumla, ni wazi unakaribisha matokezo mazuri.

Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili na cha Nne mwaka jana mara yalipotangazwa, yakazua maswali ya kijamii, hasa baada ya kubainika kuna baadhi ya wanafunzi walifanya udanganyifu na wengine waliandika lugha chafu kwenye majibu yao.

Waswahili wanasema 'Samaki Mkunje Angali Mbichi', maana akishakauka hakuna fursa ya kumkunja tena. Ni kijaribu kumkunja anavunjika, kauli hii inatafakarisha hasa kwenye malezi ya mtoto, anapaswa kujengwa kwenye msingi wa malezi bora tangu angali mdogo akikua atayazingatia.

Msingi wa malezi unafananishwa na mbegu inayopandwa na mkulima, ili kutoa mavuno mema na kuna mambo yanayopaswa kufanywa miongoni mwao, yakiwa mikononi mwa mkulima na mengine ni neema ya asili, mfano unyeshaji wa mvua.

Mimea huwa na aina ama yanayohitaji kuongezewa mbolea, pia mwanga na maji, kulingana na aina ya mbegu. Mwisho wa siku matumaini ya aliyepanda mbegu na kupitia kanuni hiyo, anaangukia mavuno mema. Ni mtiririko kama huo unamuangukia mwanadamu mwenye historia kuanzia utoto, kwenda ukubwani.

Katika asili ya maisha ya kibinadamu, pia kuna mbegu zinapopandwa, zinakosa ubora kwa sababu ya kutotunzwa vyema hivyo zinaota na kufa. Hivyo, ni umuhimu wa mbegu kutunzwa vizuri ili kulinda ubora wake.

### CHANGAMOTO YA MTIHANI

Kutangazwa matokeo ya mtihani wa kupima wanafunzi walio kidato cha pili mwaka jana, yaliyotolewa na Baraza la Mitihani ya Taifa (NECTA) ni wazi ilikuwa habari njema kwa baadhi ya wazazi, pia upande mwingine zilikuwa mbaya, kutokana na kilichotokea katika mchakato mzima kuanzia chumba cha mtihani, usahihishaji na kutangazwa matokeo.

Imetangazwa rasmi, kwamba jumla ya wanafunzi 539,645 kati ya 633,537 sawa na 85.18% wamefaulu kwa kupata alama za madaraja ya 1,11, Ill na IV.

Vilevile NECTA ilitangaza kufuta matokeo yote ya wanafunzi 14 waliobainika kuandika matusi katika majibu yao, pia hatua kama hiyo kwa wanafunzi 52 waliobainika kufanya udanganyifu.

Kwa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV, nayo yakatangazwa yakijumuisha kufutwa kwa matokeo ya watahiniwa 333, kati yao wanne wanatajwa kuandika matusi kwenye karatasi zao za majibu ya mitihani.

Kujitokeza kwa hali hiyo, hasa yakigusa matusi ni dalili inayoweza kubainisha kiwango kidogo cha nidhamu iliyopo kwa baadhi ya wanafunzi.

Hapo pia, panaibua maswali mengi, kulikoni wanafunzi hao wa kidato cha pili na nne wenye ujasiri wa kujaza matusi kwenye Mtihani wa Taifa, hatua ambayo ni 'roho; ya maisha yao ya baadaye, badala ya kuwasilisha majibu ya masomo waliyofundishwa. Ni suala linaloenda mbali sana, hata kuwatesa walimu wao kisaikolojia.

Upungufu huo wa maadili kwa namna fulani, unabainisha kuwa unachochewa na mambo mengi, ikiwamo ukaidi kati ya wanafunzi wenyewe, walimu, ndugu hata wazazi wanaotajwa kuhusika kwa namna tofauti.

### KUSUDIO LA WARAKA

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia nchini kwa kulitambua hilo, imeonyesha kukerwa na hilo na sasa inatoa Waraka wa Elimu Namba Sita wa Mwaka 2022, kuhusu Usimamizi wa Maadili kwa wanafunzi wa shule zote hizo.

Ni waraka unaolenga mambo kadhaa, ukitaka jitihada za makusudi zichukuliwe kuhakikisha kuna upatikanaji wa matokeo bora kitaaluma, ukienda sanjari na kutunza maadili. Tayari umeshanza kutekelezwa tangu Oktoba 10 mwaka jana ulipotangazwa.

Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, katika waraka huo, anaagiza utekelezwe katika shule zote za serikali na binafsi, nakala zake zikifika mbali, kwenye taasisi kadhaa, zikiwamo za kidini na elimu; wakuu wa ubora wa shule wa kanda na wilaya, ikiwataka kuisimamia na kuhamasisha utekelezaji wake.

Ni waraka unaoweza kutoa mwanya kwa watoto kujenga tabia zisizokubalika na kusababisha mmomonyoko wa tamaduni na maadili ya nchini hapa.

Ndani yake kunaelezwa kuna vyanzo vya taarifa vinavyofanya kazi ya kufundisha na kutoa malezi katika mfumo rasmi au usio rasmi, ambao imevitaja; video nyumbani, taasisi na 'vibandaumiza', kompyuta, kukinyooshewa maeneo kama michezo ya kompyuta, 'face book', instagramu 'twitter', barua pepe, na mtandao.

Vyanzo vingine ni simu za mkononi, radio, katuni, vinyago na vikaragosi, mabango mbalimbali, vitabu, magazeti, majarida na vipeperushi, mavazi, tabia na mitindo ya maisha ya watu kutoka ndani na nje ya nchi kama vile watu maarufu, wasanii na wanamichezo, makundi rika na kumbi za starehe.

### MAAGIZO YA WARAKA

Waraka umetoa maagizo 11 yanayopaswa kutekelezwa, ili kufanikisha kulinda maadili shuleni. Hiyo ni pamoja na Shule zote zianzishe au kuimarisha kamati za maadili/nidhamu shuleni, kwa usimamizi wa karibu wa walimu wakuu au wakuu wa shule, ili zifanye kazi zake za ujenzi wa tabia na maadili mema ya wanafunzi kwa ufanisi.

Pia, unataka kuimarishwa mabaraza na madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto, ili kuhakikisha suala la maadili linajadiliwa katika vikao vyote kama ajenda ya kudumu na shule zote za awali, msingi na sekondari ziweke msisitizo katika kufundishwa somo la dini, ili kuweka msingi imara wa maadili kwa wanafunzi.

Maofisa Elimu Kata, wametakiwa kushirikiana na viongozi wa vijiji/mitaa na vitongoji, kuhakikisha mazingira wanamoishi na kukulia watoto, hayana vyanzo vya taarifa zinazoharibu maadili yao, ikitolewa mfano wa kuwapo 'vibanda-umiza; vinavyoruhusu watoto kuingia na kutazama au kusikiliza mambo yaliyo kinyume nao.



Naibu Spika wa Bunge, pia Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan Zungu, katika ziara kwenye Shule ya Msingi Diamond, lengo ni kukagua hali ya mazingira na miundombinu shuleni hapo, ikiwa ni sehemu ya kufuatilia maboresho yanayofanywa shuleni. **PICHA: BEATRICE MOSES.**

ELIMU

NA DEVOTA MWACHANG'A

USHINDANI WA SHULE BORA KWENYE MIKOA TISA ...

# Mradi unaotakatisha wanafunzi chekechea hadi kidato cha sita

## • Katavi yajinasibu kung'ara ngazi zote

KISERIKALI kuna mradi wa miaka unaohusisha mikoa tisa, kupata maboresho ya kitaaluma, ukiitwa 'Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu' (EPforR II Education Program for Results II).

Zao lake sasa kushuhudiwa imeuwezesha mkoa Katavi kufanya vizuri katika sekta ya elimu, kuanzia ngazi ya awali, hadi sekondari, ukiwa na maudhui ya

kupatikana na kujifunza sawa kwa elimu bora katika ngazi tajwa.

Ni mradi unaolenga kuwa na matokeo makubwa na endelevu katika elimu kwa kusaidia kuanzisha na kuimarisha mifumo na taratibu za elimu na kwa

kufanya hivyo, anasema mpango utaimarisha matokeo ya kujifunza, hususani Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na kiwango cha wanafunzi kusalia shule.

Shule bora ni mpango na mradi wa elimu bunifu wa serikali wa miaka sita (2021-2027) katika mikoa tisa; Tanga, Dodoma, Singida, Simiyu, Pwani, Mara, Rukwa, Katavi na Kigoma, ukifadhiliwa na serikali ya Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid, unaotekelezwa katika mikoa tisa nchini.

Ni mradi unaoendeshwa, kwa msaada wa kiufundi kutoka asasi ya Cambridge Education, ikishirikiana na mashirika ya ADD international, International Rescue Committee na Plan International.



Wanafunzi wa mkoa wa Katavi, wakipatiwa sare, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha taaluma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MALENGO YA MRADI**

Bakari Geni, Mratibu wa Mradi wa Shule bora kutoka Cambrige Education Mkoa wa Katavi, ambao ni sehemu ya mradi wa Programu ya Shule Bora, wakilenga kuongeza kiwango cha usomaji kwa ufasaha, kutoka asilimia 18.9 cha mwaka 2020 hadi 25 ifikapo mwaka 2026.

Vilevile anasema, inalenga kuongeza uwezo katika somo la hisabati kutoka asilimia 17.1 ya mwaka 2020 hadi 24 mwaka 2026, huku eneo lingine analitaja ni kwa wanafunzi kusalia shule kutoka asilimia 74.25 za mwaka 2020, hadi 85 kwa mwaka 2026, huku ukizingatiwa uwiano wa kijinsia.

Mfadhili ambaye ni sehemu ya Programu ya Shule Bora, anaeleleza kuhakikishiwa watoto walioandikishwa darasa la kwanza wamalize elimu ya msingi kwa uwiano na usawa uleule.

Katika hilo, anasema mradi unataka waliomaliza shule ya msingi, waendelee na sekondari na kusiwapo hali ya kuanguka kitaaluma au kipindi cha mpito darasa la saba, hadi kujiunga na sekondari.

Geni anasema, wao wafadhili wanatilia mkazo kuwapatia fedha wahusika na kisha wafanikishe kiwango cha uandikishaji wanafunzi, kuanzia darasa la kwanza, uwe jumuishi.

Hapo anafafanua kuwa wanafunzi wote shuleni na wale waliomaliza darasa la pili kwenda la tatu, wawe wanamudu kwa ufasaha Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na mradi unaelekeza kuhakikisha watoto walioandikishwa darasa la kwanza wamalize elimu ya msingi kwa uwiano na usawa uleule.

Pia, anasema wahitimu wa elimu ya msingi, wote waendelee na sekondari na kusiwapo mdondoko kipindi cha mpito (transition) kutoka darasa la saba, kwenda kidato cha kwanza.

"Tunaendelea kufanya mabadiliko katika sekta ya elimu na kutekeleza mradi wa 'EPforR II', tumefanikiwa kupunguza mdondoko wa wanafunzi (school dropout):P," anasema Geni na kuendelea:

"Mkoa wetu (Katavi) umekuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vema. Mfano kwa mwaka jana, mkoa umefaulisha wanafunzi kidato cha sita kwa asilimia 99, wanafunzi wote wamepata sifa ya kwenda masomo ya juu."

Geni anafafanua maendeleo ya watoto na kupunguza utoro shuleni yanategemea sana ushiriki wa wazazi, hivyo uwepo wa ushirikiano wa walimu na wazazi unapozingatiwa.

"Wazazi mpambane kuzuia mazingira yanayoweza kupelekea watoto kupata madhara na kuacha masomo badala ya kusubiri hadi matokeo mabaya yatokee ndipo mjitokeze kukemea na kulaumu," anasema.

**NGAZI YA KITAIFA**

Ngazi ya taifa, Programu ya Shule Bora itatoa msaada wa kiufundi kwa serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST), Ofisi ya Rais -TAMISEMI, katika utekelezaji mradi 'EPforR II' na kufadhili matokeo muhimu yatakayotokana na vigezo, vilivyothibitishwa kutoka katika mradi ambavyo vitatumika katika kutoa fedha na wafadhili wengine.

Meneja Mawasiliano wa Mradi wa Shule Bora kutoka asasi Cambridge Education Tanzania, Raymond Kanyambo, anafafanua mradi huo unakusudia kufikia shabaha kwa kuhamasisha maboresho katika utendaji wa sekta na kuhakikisha kuna mifumo imara na endelevu katika utoaji elimu nchini.

"Mradi huu husaidia usimamizi wa matokeo (RBM) kwa kuhakikisha kuwa rasilimali zinawekwa juu ya malengo ya wazi na ufuatiliaji mzuri wa matokeo ambao unasaidia kuimarisha mifumo," anasema Kanyambo.

Anaendelea: "Mbinu ya kufadhili huhusisha kutoa fedha kwenye mipango pale tu ambapo maendeleo fulani ya malengo yaliyowekwa yanayofahamika kama viashiria vya upimaji (DLI) yanatimizwa."

Kanyambo anavieleza vipaumbele vilivyoko ni, vinavyohitaji maboresho kufikia malengo yake mahususi, katika mazingira ya ufundishaji shuleni, ili kuhakikisha shule zote za msingi zinasaidiwa kwa usawa zaidi na zinakidhi vigezo vinavyohitajika, zifanyekazi kwa ufanisi.

Anavitaja vipaumbele hivyo, ni pamoja na maboresho katika umahiri wa mwalimu na ufundishaji darasani kwa lengo kuimarisha utekelezaji wa mtaala, kupitia mafunzo endelevu ya walimu (CPD).

Lingine analitaja, ni maboresho katika mazingira ya kufundisha, ili kuhakikisha shule zote za msingi zinasaidiwa kwa usawa na zinakidhi vigezo vinavyohitajika, ili zibebe ufanisi.

**RIPOTI YA UTENDAJI**

Ripoti ya utendaji kwa mwezi Februari mwaka huu, iliyotolewa na mradi Shule Bora, inaonyesha wadau wa elimu kutoka mikoa tisa unakotekelezwa mradi wa Shule Bora kujadili ujumuishwaji wa ajenda ya 'EPforR II' katika majukwaa ya serikali na kujiwekea malengo kushiriki kutimiza viashiria vya ufanisi vilivyowekwa.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma Dk. Fatuma Mganga, anasisitiza umuhimu wa ushiriki wa wadau wote katika kuongeza kasi ya kuboresha elimu na kugeuza mradi kuwa ajenda ya kudumu katika ngazi zote za serikali.

Hapo anataja kujumuishwa kwenye ajenda za kamati za maendeleo za kata, mabaraza ya madiwani, mikutano ya mkoa na hata mikutano ya vijiji.

## WANENAVYO MALENGA

# TUPENDE WALIO HAI

1. Bora tukibadilika, uhai tuuthamini,
   Mtu homa ikimshika, tusimwache masikini,
   Tufanye ya uhakika, aimarike mwilini,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
2. Bajeti zinahusika, tiba na za msibani,
   Kile kinabainika, ni kubwa za msibani,
   Huyu aliyeondoka, kifo champa thamani,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
3. Pale alipongonjeka, kulazwa sipitalini,
   Pesa ndogo alitaka, imtoe msambweni,
   Sponsa wa kuhusika, hakutia maanani,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
4. Pesa ilipokatika, dawa kuisha njiani,
   Gonjwa likaongezeka, akafika mautini,
   Maji yameshamwagika, huwezi yazoa chini,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
5. Mbiu sasa inafika, maiti iko nyumbani,
   Michango yahitajika, kuiweka kaburini,
   Pesa zitamiminika, bila kuwa nayo soni,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
6. Nguvu hiyo ngetumika, akiwa sipitalini,
   Kifo kisingemfika, ngekimbilia dukani,
   Matibabu yangefika, akapata ahueni,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
7. Lini tutabadilika, yaingie akilini,
   Kwamba wa kuheshimika, alo hai duniani?
   Awezaye wajibika, mkikutana njiani?
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.
8. Uhai ukikatika, kaburi liko njiani,
   Vizuri kuwajibika, kwani sote tu njiani,
   Alo hai kwa hakika, huyo azidi thamani,
   Tupende walio hai, kuliko waliokufa.

**•Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com (+255) 0767223602**
**ends**

# TASAF yatoa mil.420/- kwa kaya 5,396 Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAYA 5,396 katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida zimenufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF), kwa kupatiwa Sh. milioni 420.3.

Kaimu Mratibu wa TASAF Manispaa ya Singida, Yahaya Fotta, alisema fedha zilizotolewa ni malipo ya dirisha la Septemba na Oktoba 2022, yaliyofanyika Machi 2023 na kuwataka walengwa kuzitumia vizuri kujiimarisha kiuchumi.

Fotta alisema fedha walizopewa walengwa ni nyingi hivyo wahakikishe wanazitumia kwenye miradi ya uzalishaji mali hasa katika msimu huo wa kilimo lakini pia miradi ile ya kukuza uchumi wa kaya kama ufugaji ili kuiwezesha kaya kuondokana na umaskini.

Baadhi ya wanufaika wa mfuko huo, walilalamikia kuchelewa kutolewa kwa fedha za Septemba na Oktoba na kusema kuchelewa huko kumesababisha baadhi yao kushindwa kuwahi msimu wa kilimo kwa kukosa fedha za kununua mbegu.

Mkazi wa Irao Manispaa ya Singida, Iddi Kiemi, alishauri fedha hiyo kufika kwa wakati ili kuwahi msimu wa kilimo na kujipatia chakula kitakachowakimu kwa muda mrefu.

"Nimeshachelewa msimu wa kilimo lakini fedha hizi nilizopata, nitanunua debe mbili za mahindi lakini nitalima viazi ambavyo vitahimili msimu wa kiangazi," alisema.

Pamoja na malalamiko hayo walengwa walio wengi wameishukuru serikali kwa kutoa malipo hayo ambayo yamewasaidia kununua chakula na kulipa ada za shule kwa watoto wao.

**Nimeshachelewa msimu wa kilimo lakini fedha hizi nilizopata, nitanunua debe mbili za mahindi lakini nitalima viazi ambavyo vitahimili msimu wa kiangazi.**

# Samia kufungua mkutano wa makatibu tawala mikoa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajia kufungua mkutano mkuu wa 13 wa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini (TOA) wenye lengo la kuhamasisha uwekezaji na viwanda.

Mwenyekiti wa TOA, Albert Msovela, alieleza hayo juzi jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kuhusu maandalizi ya mkutano huo kwa waandishi wa habari utakaofanyika kuanzia Aprili 4 hadi 6, mwaka huu.

"Dhima ya mkutano huu ni kuhamasisha uwekezaji na viwanda kupitia mamlaka za serikali za mitaa kwa maendeleo endelevu ambapo wadau mbalimbali kutoka serikalini na sekta binafsi wanatarajia kushiriki na mada mbalimbali zitawasilishwa," alisema.

**Taasisi hiyo inaundwa na makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wote wa mamlaka za serikali za mitaa Tanzania Bara pamoja na wanachama wengine waliopo nje ya OR-TAMISEMI.**

Kadhalika, alisema TOA imejipanga kuhamasisha usimamizi na uboreshaji wa utoaji huduma za jamii kama vile afya, elimu, kilimo, biashara, miundombinu na maji, usimamizi wa rasilimali watu, fedha, miradi ya maendeleo pamoja na utawala bora.

Vile vile, alisema taasisi hiyo inaundwa na makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wote wa mamlaka za serikali za mitaa Tanzania Bara pamoja na wanachama wengine waliopo nje ya OR-TAMISEMI.



Hata hivyo, alisema umefika wakati sasa kwa serikali za mitaa kuhakikisha wananchi wa chini ndiyo wanakuwa kipaumbele katika kuibua miradi ili kuongeza tija badala ya serikali kuu kufanya kila kitu.

Katibu Mkuu wa umoja huo, Jacob Mtalitinya, alisema pamoja na mambo mengine mkutano huo utatumika kumkabidhi tuzo Rais Samia Suluhu Hassan ya kutambua utendaji wake katika kipindi cha miaka miwili.

Alisema: "Wajumbe wa TOA kwa pamoja wamekubaliana kumpatia tuzo Rais Samia kutokana na juhudi zake za utendaji wa kazi kwa kutafuta pesa kwa ajili ya maendeleo ya nchi na wananchi wake".

Mtalitinya alisema: "Kila mtanzania anashuhudia juhudi kubwa alizofanya mkuu wa nchi kwa kuboresha sekta mbalimbali za kijamii kama vile, elimu, afya, maji, umeme na miundombinu mbalimbali ya kimaendeleo".



Mkurugenzi wa Taasisi ya Profesa Mwera Foundation ya mkoani Mara, Hezbon Mwera (kushoto), akikabidhi Tuzo ya Heshima kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, iliyotolewa na taasisi hiyo, kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango wake katika maendeleo ya sekta ya elimu nchini, wakati wa mkutano wa wadau wa elimu, jijijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Kulia ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi yamtunuku Rais tuzo ya maendeleo katika elimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAASISI ya Professor Mwera Foundation ya mkoani Mara inayojishughulisha na masuala ya elimu imemtunuku tuzo Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na mchango wake katika maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Tuzo hiyo imekabidhiwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule na Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Hezbon Mwera mwishoni mwa wiki katika mkutano wa wadau wa sekta ya elimu mkoani Dodoma.

Akizungumza kwa niaba ya Prof. Mwera, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Hezbon Mwera alisema kwa kutambua jitihada na mchango katika sekta ya elimu unaotolewa na Rais Samia wameamua kumtunuku tuzo hiyo ya heshima.

Alisema taasisi hiyo inajishughulisha na mambo ya kijamii na wamepewa kibali na Ofisi ya TAMISEMI kufanya shughuli zao ndani ya mikoa 10 ya Tanzania.

Alibainisha shughuli wanazozifanya ni pamoja na kuhamasisha vijana kujiunga na vyuo vya ufundi kwani kila mmoja anajua umuhimu wa vijana kupata mafunzo ya elimu ya ufundi baada ya kumaliza darasa la saba na kidato cha nne wakati wakisubiri matokeo.

"Nipende kumpongeza Rais Samia kwa kuanzisha vyuo katika kila wilaya, taasisi yetu hii pia inashirikiana na ofisi za mikoa kutoa tuzo kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa ya darasa la saba, kidato cha nne na sita,"alisema

Mwera ambaye pia ni Mwenyekiti wa wakuu wa vyuo vya ufundi Kanda ya Ziwa, alisema wametoa tuzo katika mikoa ya Mwanza, Kigoma, Simiyu, Shinyanga, Geita, Mara.

Pia alimkabidhi tuzo Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule pamoja na wasaidizi wake katika kuongeza ufaulu mkoani humo. Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliipongeza taasisi hiyo kwa kazi nzuri inazofanya katika sekta ya elimu kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Senyamule alisema kuwa Rais Samia amefanya jitihada kubwa kuhakikisha watoto wote wanaenda shuleni na matarajio ya serikali ya awamu ya sita ni kuona elimu bora inatolewa pamoja na changamoto zote zinatatuliwa.

Aidha, aliupongeza Mkoa wa Dodoma kwa kushika nafasi ya 10 kitaifa kwa matokeo ya mwaka 2022.

"Niendelee kusisitiza yale tutakayokubaliana tukayatekeleze, niwaombe tuzidi kupambana kuhakikisha tunafanya vizuri,"alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu, alisema wataliendeleza tukio hilo na litakuwa la kila mwaka.

Alisema ili ipatikane Dodoma yenye maendeleo lazima wawe wamoja katika kusimamia ubora wa elimu. Senyamule alisema lengo la kikao hicho ni kuangalia namna bora ya kuongeza ubora wa elimu mkoani humo na kuongeza ufaulu wa kitaifa.

Aliyataja malengo ya mkoa ni kutoka katika asilimia 83.01 mwaka 2022 hadi 85 kwa mwaka 2023 katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi.

Pia, alitaja lengo la pili ni kutoka asilimia 91.27 mwaka 2022 hadi asilimia mia mwaka 2023 katika upimaji wa elimu kitaifa katika darasa la nne.





# TAKUKURU yabaini upungufu kwenye miradi ya bil.71/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imebaini upungufu kwenye miradi 75 ya Sh. bilioni 71.8 kabla ya miradi hiyo kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Hayo yamebainishwa juzi na Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Vangseda Mkalimoto alipotoa taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo kwa kipindi cha robo ya mwaka.

Alisema sekta ambazo zimebainika kuwa na dosari ni elimu, afya, maji na miundombinu ikiwemo barabara na kufafanua kuwa miongoni ni Shule ya Sekondari Santilya iliyopo wilayani Mbeya ambayo ilipewa Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

**Baada ya kufanya uchunguzi walibaini upungufu kwenye moja ya chumba ambacho ujenzi wake haukuridhisha.**

Hata hivyo alisema baada ya kufanya uchunguzi walibaini upungufu kwenye moja ya chumba ambacho ujenzi wake haukuridhisha.

Alisema kwa kuzingatia miiko na utaratibu wa kazi walikaa na uongozi wa sekondari hiyo ili kujua kwa nini kuna dosari kwenye ukamilishaji wa moja ya darasa shuleni hapo na yakafanyiwa kazi kwa haraka.

Aliongeza kuwa walibaini mapungufu kwenye ujenzi wa Barabara ya Hatwelo- Igawilo yenye urefu wa kilometa tano, inayogharimu Sh. milioni 80 ilianza kuharibika kabla mkandarasi hajakabidhi kwa serikali.

"TAKUKURU pia tulifanya ukaguzi kwenye mifumo ya uendeshaji wa hospitali na vituo vya afya wilayani Mbarali na kubaini mapungufu kwenye upatikanaji wa uvifaa tiba licha ya kuwa serikali ilishasambaza kwenye maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za matibabu sambamba na wahudumu kutoa lugha chafu kwa wagonjwa,"alisema Mkalimoto.

Hivyo, aliwasihi wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo juu ya viashiria vya rushwa ili kuisaidia miradi ya serikali miradi kutekelezwa kwa ufanisi kama ilivokusudiwa.

# BoT yatoa elimu ya utambuzi noti halali, bandia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BENKI Kuu Tanzania (BoT) mkoani Mbeya, imetoa elimu kwa makundi mbalimbali kwenye jamii kwa lengo la kuzifahamu shughuli zinazofanywa na benki hiyo.

Juzi Mtaalam wa Uchumi wa BoT Mbeya, Dk. Nicholous Kesi alitoa elimu kwa wanachuo, wafanyakazi na wahadhiri wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) matumizi ya sarafu na namna ya kuzitambua noti halali na bandia.

Alisema wapo baadhi ya watu ambao siyo waaminifu wanafanyabiashara ya kuzalisha noti bandia na matokeo yake huwabambikizia watu ambao pasipo kuzitambua huzitumia kwenye manunuzi na baadae kupata kesi za utapeli na wizi.

Hivyo, aliwashauri wanafunzi wa vyuo vikuu kutorubuniwa na watu ili kuingia kwenye uzalishaji wa noti bandia kwa madai kuwa anayebainika hufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

"Tuna utaratibu wa kutoa elimu kwa makundi mbalimbali katika jamii yetu lengo ni watu kufahamu shughuli zinazofanywa na BoT, wengi wanajua sisi ni kuhifadhi fedha zilizoharibika lakini wanasahau kwamba tunaelimisha kuhusu noti halali na bandia, kuzisaidia taasisi za fedha, lakini pia kutoa nafasi wananchi wanaotaka kuweka hisa zao benki," alisema Dk. Kesi.

Kaimu Mkuu wa MUST,Profesa Godliving Mtui alisema bado kuna uhitaji mkubwa wa elimu ya fedha hususani masuala ya fedha mtandao.

Aliongeza kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu mbali ya fani wanazosomea wanapaswa kujifunza masuala ya fedha ili wasijiingize kwenye mikopo isiyo na tija.

Mhadhiri Msaidizi wa MUST, Magreth Giga alisema elimu hiyo itawasaidia katika utambuzi wa alama zilizopo kwenye utunzaji wa fedha, kufahamu mifuko na thamani ya fedha.



Mwanasheria wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Envirocare linalojihusisha na uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira na jinsia, Godlisten Muro (kushoto), alitoa elimu ya kilimo cha kahawa na umuhimu wa upangaji bajeti kwa kuzingatia mlengo wa kijinsia kwa wakazi wa kijiji cha Malowe, wilayani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waandishi wa habari Mbeya wakusanya mil.12/- miezi mitatu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KIKUNDI cha kuweka na kukopa cha waandishi wa habari mkoani Mbeya (MBPC), katika kipindi cha Januari mpaka Machi 2023, kimekusanya zaidi ya Sh. milioni 12 kama hisa kutoka kwa wanachama wake.

Akitoa taarifa ya mapato na matumizi ya kikoba hicho mwishoni mwa wiki, Mtunza Hazina, Elizabeth Nyivambe alisema wastani wa makusanyo ya hisa kwa wiki ni Sh. 900,000 na wanachama kila mmoja ananunua hisa moja hadi tano.

Alisema kikundi hicho kimeweza kutoa mikopo ya Sh. milioni nane kwa wanachama wake.

Aliongeza kuwa wanachama wamekuwa waaminifu kwenye urejeshaji wa mikopo yao hali inayosaidia kuwa na akiba ya fedha na kusaidia wengine wenye uhitaji wa kukopa kuzipata kwa wakati.

"Nawapongeza wanachama wenzangu wa kikoba tunakwenda vizuri na kila mmoja anaona faida ya kuingia kwenye kikundi hiki imetujengea nidhamu ya matumizi ya fedha," alisema Elizabeth.

Januari 7 mwaka huu, Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson alizindua rasmi kikundi hicho hafla ambayo ilihudhuriwa pia na Waziri wa Habari, Nape Nnauye ambaye aliwaahidi kuwapatia Sh.milioni 100 kwa ajili ya kutunisha mfuko.

Wakati akizindua kikundi hicho Dk. Tulia alichangia Sh. milioni 15 ambayo ilikopeshwa kwa wanachama 33 kila mmoja akipata Sh. 500,000 ambazo zote zitarejeshwa Julai mosi mwaka huu.

Mmoja wa wajumbe wa kikoba hicho, Emmanuel Lengwa alipendekeza sehemu ya faida watakayoipata kupitia gawio itumike kulipa ada ya klabu ya waandishi wa habari Mkoa wa Mbeya ambapo kila mwanachama hulipia Sh. 40,000 pendekezo ambalo lilikubaliwa na wanachama wote.

Mweyekiti wa kikoba hicho, Ezekiel Kamanga alisema mwaka 2022, kikundi hicho kilikusanya zaidi ya Sh. milioni 21 ambazo walikopeshana na kugawana faida, wanachama walipata faida kati ya Sh. 100,000 hadi Sh. milioni mbili.

Aidha, aliwapongeza viongozi wenzake kwa kushirikiana pamoja na kusimamia sheria na kanuni zilizowekwa kwa ajili ya kuendesha kikoba hicho ambacho kwa sasa kimekuwa mkombozi kwa wanahabari wa Mkoa wa Mbeya.





# CCM: SUK imeimarisha demokrasia, umoja kitaifa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimesema Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) imesaidia kuimarisha misingi ya demokrasia na umoja wa kitaifa kwa wananchi wa Zanzibar.

Hayo yalielezwa juzi na Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufika katika Hospitali ya Al- Rahma kumjulia hali aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maridhiano, Ali Mzee Ali.

Alisema kwamba tangu kufanyika kwa marekebisho ya 10 ya Katiba ya mwaka 1984 na baadae kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa siasa za chuki zimetoweka na misingi ya umoja wa kitaifa ikiendelea kuimarika visiwani Zanzibar.

"Nimekuja kumjulia hali mwanasiasa mkongwe, Ali Mzee baada ya kusikia amelazwa hospitali, huyu ni mtu muhimu sana kwa Zanzibar amesaidia kujenga misingi ya demokrasia na umoja wa kitaifa kutokana na kazi nzuri aliyoifanya," alisema Mbeto.

Alisema kwamba Zanzibar sasa inashuhudiwa siasa ya kistaarabu kwa wanachama na vyama vya siasa vikishindana na kukosoana kwa hoja badala ya siasa za chuki na uhasama.

Aidha, alisema miradi ya maendeleo inayoendelea kujitokeza Zanzibar katika sekta ya elimu, afya, miundombinu na sekta zingine imetokana na kuimarika kwa hali ya amani na usalama nchini.

Hata hivyo alisema kwamba wananchi wanapaswa kuheshimu na kuenzi Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo ndiyo chimbuko la amani inayoendelea kutawala visiwani Zanzibar tofauti na miaka ya nyuma baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi.

Akizungumza akiwa amelazwa hospitali hapo, Ali Mzee, alisema anaendelea vizuri baada ya kupatiwa matibabu tangu alipolazwa Machi 25 mwaka huu.

"Hali yangu inaendelea kuimarika tangu nilipoanza kupatiwa matibabu, nawashukuru kwa kufika kunijulia hali wakiwemo viongozi wa kitaifa"alisema Mzee.

Kada wa CCM, Saleh Mohamed Said, alisema kwamba amefika kumjulia hali mwanasiasa huyo baada ya kupokea taarifa kuwa amelazwa hosptali akisumbuliwa na matatizo ya kiafya.

# Serikali yaagiza kuondolewa ombaomba mitaani Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imewaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa manispaa na halmashauri kupambana na vitendo viovu vinavyofanywa katika maeneo yao ikiwamo kuwaondoa ombaomba.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed, alitoa maagizo hayo jana ofisini kwake Vuga wakati akizungumza na wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa mabaraza ya miji na halmashauri.

Alisema imejitokeza hali isiyokuwa ya kawaida kwa baadhi ya wananchi kujikusanya pembezoni mwa barabara na wengine kukaa kwenye nyumba za ibada kufanya biashara ya kuomba hali inayoitia doa serikali.

Aidha, aliwataka wakuu hao kusimamia zoezi hilo kuwaondosha watu hao kwa utaratibu unaofaa ikiwemo kuwarejesha katika maeneo yao.

**Agizo hilo halitohusisha shughuli za harusi na siku ya kuzaliwa ambazo hazina muendelezo wa ngoma kwa siku zote kama zilivyo nyumba za kulala wageni na hoteli.**

"Unapofika mwezi kama huu wa Ramadhani hujitokeza watu ambao huwakusanya watu wenye ulemavu wa viungo na watoto kwa kuwatumia kwa biashara ya ombaomba kwa kukaa karibu na barabara kuu na nyumba za ibada na kutia doa serikali yetu" alisema Masoud.

Aidha, alisema utaratibu huo unakwenda kinyume na mila, desturi za mzanzibar, hivyo aliitaka jamii kufanya shughuli nyengine na kuacha biashara hiyo.

Akizungumzia kuhusu dawa za kulevya aliwataka wakuu hao kufanya operesheni za mara kwa mara za kupambana na watu wanaojihusisha na biashara hiyo kulinusuru taifa.

"Bado wapo wafanyabiashara wa dawa za kulevya ninachowaomba nendeni mkafanye operesheni kuondosha biashara hii", alisema.

Akizungumzia kuhusu upigaji wa muziki katika nyumba za kulala wageni na hoteli za kitalii aliwataka wamiliki wa nyumba hizo kuweka vizuia sauti kuepusha migogoro kati yao na wananchi.

Hata hivyo aliwaagiza wakuu hao kutokubali kutoa vibali kwa wamiliki wa nyumba za kulala wageni ambao hawafuati taratibu kuepusha migogoro inayoendelea kujitokeza kila siku.

Alisema agizo hilo halitohusisha shughuli za harusi na siku ya kuzaliwa ambazo hazina muendelezo wa ngoma kwa siku zote kama zilivyo nyumba za kulala wageni na hoteli.

Akizungumzia maelekezo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka, alisema watayafanyia kazi maagizo hayo na kuahidi kufanya zoezi hilo katika kipindi kifupi.



Katibu wa Kamati Maalum ya NEC ya CCM Idara ya Itikadi na Uenezi Zanzibar, Mbeto Khamis Mbeto (kulia), akimjulia hali Mwanasiasa mkongwe visiwani Zanzibar ambaye alikuwa Mwenyekiti wa kamati ya mariadhino, Ali Mzee Ali alipomtembelea katika hospitali ya Al-Rahma, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja hivi karibuni. Kushoto ni mfanyabiashara maarufu Zanzibar na kada wa CCM, Saleh Mohamed Said. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'SMT, SMZ kupunguza umaskini, kuongeza ukuaji uchumi'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISA Mdhamini Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Pemba, Abdullwahab Said Bakari, amesema miongoni mwa malengo ya Serikali ya Tanzania (SMT) na Serikali ya Zanzibar (SMZ) ni kupunguza umaskini kwa wananchi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Alisema serikali imepanga mpango wa kupunguza umaskini na kuongeza ukuaji wa uchumi jumuishi unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) ambayo imeweka sifa kwa walengwa wake.

Mdhamini huyo aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa masheha na madiwani wa Mkoa wa Kusini Pemba yaliyohusu kuwajengea uwezo viongozi wanaosimamia shughuli za TASAF.

Alisema matumaini ya TASAF kwenye mafunzo hayo, masheha watakua ndiyo masikio mazuri ya kusikiliza changamoto za walengwa wa mpango na wanakabiliana nazo.

"Hivi sasa kuna changamoto nyingi kutoka kwa walengwa, masheha na madiwani mtakuwa ni mabalozi, pia mtakuwa ni wasemaji wazuri wa kuisemea TASAF kwa jamii", alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF Tanzania, Mkurugenzi wa Uratibu, Haika Shayo, alisema mafunzo hayo yatasaidia kufanikisha lengo la mpango na kutakuwa ni mwanzo mzuri kwa viongozi hao kufahamu kikamilifu shughuli mbalimbali za TASAF.

Aidha, aliwataka walengwa kuhakikisha wanafungua akaunti benki kwa ajili ya kupokea fedha zao, kwani suala la fedha mkononi limeshaondoka," alisema.

Ofisa Ufuatiliaji TASAF Pemba, Abrahman Khamis, alisema madhumuni ya mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo viongozi wanaosimamia shughuli za mpango, kuwa na uelewa juu ya taratibu zinazotumika kusimamia na kufuatilia shuhuli za mpango.

Mratibu wa TASAF Pemba, Mussa Said, alisema lengo ni kuongeza kipato kwa wananchi, pamoja na kuongeza ujuzi kupitia miradi wanayoianzisha kwenye maeneo yao, kwamba ushirikishwaji wananchi ni jambo kubwa katika kuibua miradi ya maendeleo kupitia walengwa wa mpango wa kunusuru kaya masikini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ORDINANCE [CAP.117]**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED, I**, the underdesigned, **RAYMOND ALEX MASAKI** of Dar es salaam Region and a citizen of Tanzania **DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly **RENOUNCE RELINQUISH** and **ABANDON** the use of my former names **RYMOND MASAKI**; as appearing in my other parastatal pension Fund documents and records, deeds and other documents and in lieu thereof do assume the name **RAYMOND ALEX MASAKI** as appears in my National Identity Card issued by **NIDA.**

**AND** for the purpose of evidence of such determination, I Hereby **DECLARE** that I shall at all times herein after in all records, deeds and instruments in writing and in all actions proceedings dealings and transactions upon all occasions whatsoever in public and private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the assumed names **RAYMOND ALEX MASAKI** instead of the names renounced.

**AND** the reason for abandoning my old names **RYMOND MASAKI** is to put my records clear and maintaining uniformity in all my records.

**AND I HEREBY AUTHORISE** and request all persons to address me by such assumed names instead of the names renounced.

**IN WITNESS WHEREOF,** I have set my hand at Dar es Salaam, and hereof substitute my old names above with my name of names **RAYMOND ALEX MASAKI.**

DEPONENT

COMMISSIONER FOR OATHS



## KUPOTEA KWA CHETI



**SALIMU SELEMANI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S555/0042** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BUNGU SECONDARY SCHOOL** mwaka 1998. Kwa yeyote atakaeliona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/116710/2023**

**TANZANIA**

Certificate of Incorporation of a Company

Section 15

NO:153349967

I HEREBY CERTIFY THAT

**NORRIS TRANSPORT LIMITED**

Is this day incorporated under the companies Act, 2022 and that the Company is limited

**GIVEN** under my hand at Dar es salaam this 9th day of **SEPTEMBER TWO THOUSAND AND TWENTY ONE.**

PRINCIPAL REGISTRAR OF COMPANIES

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KHALID AME MACHANO** anatangaza kupotelewa na card ya Gari aina ya **Toyota Porte** yenye namba za usajili **T443CTL,** Chassis namba: **NNP110009329** Engine namba: **1NFE4172** Rangi ya Pearly White. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi kilichopo jirani yako. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/116297/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MDILI SAMBAYI KATEMANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 403 DDF – NISSAN BLUE-BIRD.** Chassis No. **KG11067605.** Engine **No. MR20476863A.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/118612/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Mdai 17, 2023**
**Jina la Mdai Geofrey John Mongi**
**Jina la Mdaiwa Sia Alexanda Ngowi**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa: SIA ALEXANDA NGOWI**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )**

Mdai anadai talaka dhidi yako hivyo fika mahakamani kuskiliza madai hayo

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 14 mwezi 04 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 31 mwezi 03 Mwaka 2023

Magistrate Court (Approved Forms for the Primary Court.)

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Mahakama ya Mwanzo Mafinga tutauza mali za wadaiwa kama ifuatavyo:

**MADAI.....No 30/2022**
- **SHAABAN SPOMPUTA........MDAI**
- **ISAYA GREGORY NYEHO......MDAIWA**

Kiwanja kilichopo **MET-MAFINGA MJINI KITALU A-BLOCK No.47.**

Kitauzwa Tarehe 21.04.2023 na Mnada utafanyika saa 5 kamili Asubuhi.

**MASHARTI YAMEANDIKWA KATIKA MBAO ZA MATANGAZO.**

**KWA MAWASILIANO:**
**0748 237245**
**0764 464746**
**0764 430413**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CLEMENCE AUGUSTINO MBILANGO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 391 DRY** na pleti namba yake,aina ya pikipiki ni TVS, kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

**MOR/MOR/RB/117110/2023**


## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**

# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Raila Odinga atangaza kusitishwa maandamano

**NAIROBI, Kenya**

KIONGOZI wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, ametangaza kusitisha maandamano ya kupinga gharama za maisha yaliyopangwa kufanyika jana ili kutoa nafasi ya mazungumzo na Serikali.

Uamuzi huo umekuja baada ya Rais wa nchi hiyo, William Ruto kusema kwamba yupo tayari kushirikiana na wapinzani ili kutatua changamoto hiyo.

Kenya imekuwa katika maandamano kwa wiki mbili sasa ambayo yamesababisha uharibifu mkubwa wa mali huku mamia ya raia wakiripotiwa kujeruhiwa wakiwemo maofisa wa polisi na waandishi wa habari.

Kufuatia hali hiyo, Rais William Ruto katika hotuba yake kwa taifa alitoa wito kiongozi huyo wa upinzani, kusitisha maandamano hayo na kukubaliana na mojawapo ya matakwa yake ya ushirikiano wa pande mbili bungeni kuhusu kuundwa kwa tume mpya ya uchaguzi.

"Nimesikiliza kwa makini masuala yaliyoibuliwa na rafiki yangu Raila Odinga na nyakati kama hizi sio wakati wa kuangalia nani yuko sahihi au nani amekosea, mara zote nimekuwa tayari kuzungumza na raia wote bila kubagua kuanzia viongozi waliochaguliwa kisiasa hadi wa dini ili tujadiliane namna tutaijenga nchi yetu," alisema Rais William Ruto.

Odinga alisema wapo tayari kwa mazungumzo na wataendelea kufanya hivyo kama Rais Ruto na serikali yake wapo tayari kwa sababu wanataka suluhu ya amani kwa tofauti walizo nazo katika nchi hiyo na kuimarisha demokrasia.

"Tunataka uchaguzi wetu uwe na maana, lakini katika kufanya hivyo tunataka kusisitiza kuwa haki ya kukusanyika, kuandamana, kuwasilisha malalamiko na kupaza sauti ni mambo ambayo yapo kikatiba" alisisitiza Odinga. ***RFI***



Watu wakitembea kwenye maji ya mafuriko kwenye mji wa Quelimane, Msumbiji baada ya kushambuliwa na kimbunga Freddy. **PICHA:MTANDAO**

# DPP atakiwa kueleza hatua walizochukua dhidi ya wanahabari walioshambuliwa

**NAIROBI, Kenya**

SHIRIKISHO la Wanahabari nchini Kenya, limetoa siku saba kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP) kutoa taarifa kuhusu hatua walizochukua kwa polisi na watu waliohusika kuwashambulia na kupora vifaa vya kazi vya waandishi habari waliokuwa wakiripoti maandamano yaliyoitishwa na upinzani.

Kauli yao imekuja saa chache tangu wanasiasa wa mrengo wa chama tawala kutoa matamshi yaliyotafsiriwa kama kitisho kwa uhuru wa vyombo vya habari.

Akizungumza kwa niaba ya waandishi wa habari nchini humo Katibu mkuu wa shirikisho hilo, Erick Oduor, alisema wanataka kufahamu kama kumeshafanyika uchunguzi juu ya suala hilo lililofanyika jumatatu iliyopita na ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wahusika.

"Tuna ujumbe kwa mwendesha mashataka, kutueleza ni hatua zipi wamechukua dhidi ya watu waliowashambulia na kuharibu vifa vya wanahabari, tunawapa siku saba kufanya hivyo. Iwapo serikali itashindwa kufanya hiyo kazi basi tutasusia kutoa habari za serikali," alisema Erick Oduor.

Katika hatua nyingine, Rais William Ruto, amesisitiza serikali yake haiungi mkono vitendo vyovyote vinavyotishia uhuru wa habari akisema wataendelea kutoa ushirikiano.

"Kama kulikuwa na vitendo vyovyote vya makusudi kumshambulia mwanahabari naweza kukwambia hapa kuwa tunavipinga kwa sababu tunaamini kuwa vyombo vya habari lazima viachwe huru kutimiza majukumu yao," alinukuliwa Rais William Ruto.

Alisema serikali inaamini katika uhuru wa vyombo vya habari hivyo kitendo chochote ambacho kitamueka mwanahabari katika hatari hakikubaliki. Wanahabari wameripotiwa kujeruhiwa na vifa vyao vya kazi kuharibiwa na waandamanaji na maofisa wa polisi wakati walipokuwa katika harakati zao za kila siku za kuangazia maadamano ya upinzani nchini kenya.

Tukio hilo la kusikitisha limeibua hisia kutoka kwa wadau mbalimbali wa habari ikiwamo Baraza la Habari Tanzania (MCT) waliolaani vikali vitendo hivyo kwa madai kuwa vinahatarisha usalama wa waandishi habari nchini humo

Taarifa iliyotewa na Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, ilieleza kuwa ukiukwaji huo unafaonywa na watendaji wa serikali na wasio wa serikali unahatarisha maisha na usalama wa wataalam katika vyombo vya habari nchini humo.

"MCT inapenda kutoa wito kwa wahusika wote katika mazingira ya kisiasa ya Kenya kuzidisha vizuizi na kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Wakati huo huo, kiongozi wa chama pinzani nchini humo , Raila Odinga amesitisha maandamano yaliokuwa yamepangwa kufanyika jana kama njia moja ya kutoa nafasi ya kufanyika kwa mazungumzo na serikali.

***RFI***

## Maelfu waugua kipindupindu Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

Wiki kadhaa baada ya kimbunga Freddy kuingia Msumbiji kwa mara ya pili, taifa hilo linashuhudia ongezeko kubwa la maambukizi ya kipindupindu kutokana kuwapo kwa mafuriko yaliyosababishwa na kimbunga hicho.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AP, kufikia Machi 27 mwaka huu , zaidi ya visa 19,000 vya kipindupindu vilikuwa vimeripotiwa katika mikoa yote nane huku ripoti kutoka ofisi ya Umoja wa Mataifa (UN) inayoratibu masuala ya kibinadamu ikisema kumekuwa na ongezeko maradufu ndani ya wiki moja.

Watu 31 wameripotiwa kufa kwa ugonjwa huo kwenye hospitali ya mji mkuu mkoa wa Zambezia wa Quelimane , huku wengine 3,200 wakilazwa hospitalini kati ya Machi 15 na 29 kulingana na tawimu za wizara ya afya.

Kimbunga hicho kinachosemekana kuwa kirefu zaidi kikichukua zaidi ya wiki 5 na kugonga Msumbiji mara 2, kiliuwa watu 165, Msumbiji, 17 Madagascar na 676 nchini Malawi. Zaidi ya watu 530 kufikia sasa hawajulikani walipo nchini Malawi na huenda idadi ya vifo nchini humo ikapita 1,200.

***VOA***

## 19 wafariki katika maporomoko ya ardhi mashariki mwa DRC

**KINSHANSA, DRC**

MAPOROMOKO ya ardhi yanaelezwa kuwa yameua watu 19 mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, siku ya jumapili, maofisa wa eneo hilo wamesema.

Kwa mujibu wa kiongozi wa Kijiji Cha Bulwa, wilayani Masisi, Chadrack Mbukanirwa Ndibanja, maafa hayo yalitokea majira ya asubuhi katika jimbo la Kivu Kaskazini na uokoaji uliendelea hadi jana.

Kiongozi mwingine wa eneo hilo, Alphonse Musheba Mihingano, alithibitisha kwamba miili 19 ilipatikana lakini akasisitiza kuwa idadi hiyo ya vifo ni ya awali.

Alisema kinamama 25 na watoto wao, walikuwa wanafua nguo kwenye mto chini ya mlima wakati udongo ulipoporomoka na kuwafukia baadhi yao.

Mkazi wa kijiji cha Bulwa, Musafiri Balume, alisema amepoteza dada yake katika maporomoko hayo ambayo yalitokea wakati wa mvua kubwa.

***VOA***

HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA BADO POINTI TANO KUREJEA TENA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 4-0 ilioupata JKT Tanzania kwenye uwanja wake wa nyumbani, Meja Jenerali Isamuhyo dhidi ya Mbuni FC, umeifanya timu hiyo kuhitaji pointi tano tu kuweza kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara.

Maafande hao ambao waoliteremka msimu wa 2020/21, walipata ushindi huo juzi kupitia wafungaji wao Maka Edward dakika ya 14, Edward Songo akifunga mawili dakika ya 35 na 55, pamoja na Edson Katenge dakika ya 44.

Kutokana na ushindi huo, JKT Tanzania sasa wanafikisha pointi 59, ambapo wanahitaji alama tano tu kufikisha jumla ya pointi 64 ambazo hazitafikiwa na timu yoyote kwenye Ligi ya Championship msimu huu.

JKT Tanzania imebakisha mechi nne tu ambapo kama itashinda michezo miwili iliyobaki moja kwa moja itakuwa imerejea Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu ya Kitayosce inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo, ililazimishwa suluhu na Pamba FC katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza na kuzifanya timu hizo kuwa kwenye vita kali ya kuwania kupanda Ligi Kuu.

Kitayosce imefikisha pointi 50 ikibakisha mechi nne ambazo ikishinda itafikisha pointi 62, Pamba FC iko nafasi ya tatu kwa pointi zake 48, lakini yenyewe imebakisha mechi tano na kama ikishinda zote itakuwa na pointi 63.

Kwa maana hiyo kati ya timu hizo tatu, mbili zitapanda na moja itatakiwa kubaki kwenda kucheza mechi za mchujo.

Mbali na mechi hizo, kwenye Uwanja wa Majimaji Songea, Mbeya Kwanza ililazimishwa suluhu dhidi ya Green Warriors, Fountain Gate ikaiadhibu African Sports mabao 2-0 kwenye Uwanja wa CCM Gairo mkoani Morogoro, KenGold ikilazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Ndanda, Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga na kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, Biashara United, ililazimishwa suluhu dhidi ya Transit Camp.

ZAWADI...




Meneja Masoko wa Benki ya KCB Tanzania, Shose Kombe (kushoto), akikabidhi zawadi kwa mshindi wa kwanza wa michuano ya pikipiki ya Kilimanjaro Vasso Motorbike 2023, yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki na kupewa udhamini na benki hiyo. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Singida BS yautaka ubingwa FA

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Singida Big Stars ya mkoani Singida imejigamba kuwa imejipanga kikamilifu katika mchezo wa nusu fainali wa Kombe la Shirikisho la Soka la Azam (ASFC), maarufu FA Cup, kuhakikisha wanafanikiwa kutwaa taji hilo msimu huu.

Singida Big Stars imefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya FA baada ya kuitandika Mbeya City kwa mabao 4-0 katika mchezo wa robo fainali ya FA uliochezwa juzi katika Uwanja wa CCM Liti, hivyo inasubiri timu itakayofuzu hatua hiyo kati ya Yanga na Geita Gold FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, amesema wamefurahi kufika hatua hiyo na kwamba wamejipanga kukutana na timu yoyote katika hatua ya nusu fainali ili kufikia malengo ya kutwaa kombe hilo.

"Tunashukuru Mungu tumepata matokeo mazuri sana, hatukutarajia kuifunga Mbeya City magoli manne, si kitu kidogo kuifunga magoli hayo hasa kwenye mashindano makubwa kama haya, ni ushindi mnono, hii inatokana na matokeo chanya ya kambi tuliyoiweka Dodoma.

"Tulijiandaa vya kutosha hata uchezaji wa leo 'juzi', ulionesha kwamba ni timu iliyojiandaa, hivyo tunaenda kwenye nusu fainali tukijiamini kwa kiasi kikubwa, hata benchi la ufundi linaona mafunzo wanayoyatoa yameeleweka kwa wachezaji, tupo tayari kwa nusu fainali.

"Hatua tuliyofikia hivi sasa tunaweza kukutana na Yanga ama Geita Gold, hivyo tupo tayari kucheza na timu yoyote ile, timu zilizoingia robo fainali zote ni ngumu na nzuri, tunaamini kila tutakayekutana naye atakuwa mpinzani mzuri, tunahitajia kufika fainali na hatimaye kutwaa taji hilo," alisema Massanza.

Hatua hiyo ya robo fainali iliendelea tena jana kwa Azam FC kuvaana na Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamanzi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam ambapo mshindi wa mechi hiyo atakutana na mshindi kati ya Simba na Ihefu FC itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Uhuru.

## Droo 16-bora FA Cup Z'bar J'tatu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

DROO ya hatua ya 16-bora ya Michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanziba (ZFF), maarufu FA Jumatatu ijayo, Aprili 10 visiwania hapa.

Katika droo hiyo, itakwenda sambaba na ile ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kwa Kanda ya Pemba.

Kwa upande wa Kanda ya Unguja timu zilizotinga hatua ya 16-bora ni Villa United, Kundemba FC, JKU SC, Muungano Ranger, Black Sailors, New King, Mafunzo SC, Dulla Boys, Mwembeladu FC, Raskazone, New City, New Boys, Uhamiaji FC, KMKM SC, M/Makumbi City na Mlandege.

Na kwa upande wa Kanda ya Pemba timu nane zilizotinga robo fainali ni Tekeleza FC, Mkoroshoni FC, Al Azzar FC, Maendeleo United, Machomane United, Jamhuri FC, Young Islanders na Chipukizi FC.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ZFF, Ali Bakar 'Cheupe', alisema michuano hiyo kwa hatua ya 16-bora kwa Kanda ya Unguja na robo fainali kwa Kanda ya Pemba itaanza kutimua vumbi Mei 2 hadi Mei 5 mwaka huu.

## Zahera akalia kuti kavu Polisi Tanzania

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Mwinyi Zahera, amekalia kuti kavu kuendelea kuinoa timu hiyo iwapo hatafanikisha kuibakisha Ligi Kuu Bara kuelekea msimu ujao wa 2023/24, imeelezwa.

Polisi Tanzania inashikilia mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 19 baada ya mechi 25 ilizocheza mpaka sasa huku ikibakiza michezo mitano tu kabla ya ligi hiyo msimu huu kutamatika na Zahera amepewa jukumu la kuhakikisha anaibakiza timu hiyo kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Frank Lukwaro, alisema moja ya makubaliano ambayo waliingia na Zahera wakati wanasaini mkataba wa kuinoa timu hiyo ni kuhakikisha anaibakisha Polisi Tanzania kwenye ligi hiyo. "Malengo tuliyokubaliana na kocha Zahera ni kuhakikisha timu inasalia Ligi Kuu, lakini bado hatujafikia hilo lengo, hivyo hatuwezi sema tupo vibaya sana au vizuri na hizo mechi tano zilizobakia kocha amesema aamini hatashuka.

"Bado tunaendelea kusubiri kuona ni kwa jinsi gani tunafikia hilo lengo la kuibakisha timu Ligi Kuu, siwezi sema kama tutaachana naye au tutabaki naye kwa malengo ambayo tumejiwekea ni kuhakikisha timu inabaki na yeye analitambua.

## ZISIKUPITE

### BENITEZ ATAJWA LEICESTER

RAFAEL Benitez, Jesse Marsch, Ralph Hasenhuttl na Adi Hutter wote wanawania nafasi iliyo wazi ya kocha wa Leicester City. ***(Mail)***

### LINDSTROM AWINDWA LIVER

LIVERPOOL inavutiwa sana na mchezaji wa Eintracht Frankfurt na kiungo wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom, mwenye umri wa miaka 23, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal. ***(Florian Plettenberg - Sky Sports Germany)***

### POTTER KUMRITHI RODGERS

KUFUKUZWA kwa Graham Potter na Chelsea kutaibua shauku kubwa katika Klabu ya Leicester City, huku kocha huyo akitajwa kuwa mrithi wa Brendan Rodgers. ***(Leicester Mercury)***

### SILVA NAYE AHUSISHWA

KOCHA wa Fulham, Marco Silva ameibuka kama mgombea wa kushtukiza wa kuwa kocha wa Chelsea. ***(Mirror)***

### NAGELSMANN NA CHELSEA

CHELSEA inavutiwa na kocha wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, baada ya kumfukuza Potter, wakati kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino pia ana mashabiki kwenye bodi. (Sport)

### GALLAGHER ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL imemtambua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, kama shabaha yao kuu msimu huu. (Independent)

### ARSENAL YATAKA WATATU

ARSENAL inawalenga wachezaji watatu katika safu ya kiungo msimu huu wa majira ya joto akiwamo mchezaji wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 21, Moises Caicedo (21), na mchezaji wa West Ham na England, Declan Rice, 24. ***(Football Insider)***

### MADDISON AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inataka kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na England, James Maddison mwenye miaka 26. ***(Football Insider)***

### JAMES KUZUIWA MADRID

CHELSEA inajiandaa kuzuia nia ya Real Madrid kumnunua mlinzi wa England, Reece James, mwenye umri wa miaka 23, msimu huu na wanaweza kutoa kiasi cha pauni milioni 90. ***(Football Insider)***

### SALISU ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa ni mahali pazuri zaidi kwa beki wa Southampton na Ghana, Mohammed Salisu, mwenye umri wa miaka 23, ambaye ana thamani ya pauni milioni 25, kuliko Chelsea na Manchester United. ***(Mail)***

## DONDOO SOKA MAGAZE LAYA



# TEN HAG AKUBALI UNITED ILISTAHILI KIPIGO NEWCASTLE

Sipendi kusema, lakini walikuwa bora zaidi, lazima uwe na njaa, lazima utoe kila kitu, kila mchezo...

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag anaamini Newcastle "ilitaka kushinda zaidi" kuliko Manchester United juzi, Jumapili.

'Mashetani Wekundu' hao waliteleza na kupata kipigo cha pili katika mechi zao tatu zilizopita za Ligi Kuu England walipofungwa 2-0, mabao ya kipindi cha pili ya Joe Willock na Callum Wilson kwenye Uwanja wa St James' Park yakiwa kama kulipiza kisasi kwa kupoteza mchezo wa fainali ya EFL kwa United.

United imeshuka hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu kwa matokeo hayo, nyuma ya Newcastle kwa tofauti ya mabao na pointi moja pekee mbele ya Tottenham Hotspur.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Ten Hag alikiri kuwa timu yake ilistahili kupoteza.

"Sipendi kusema, lakini walikuwa bora zaidi leo (juzi)," alisema akiiambia Sky Sports.

"Hasa dhamira yao, shauku na nia. Walitaka kushinda zaidi wiki hii, kwa hivyo walishinda.

"Nadhani tulikuwa na nafasi zetu, lakini lazima uelekee golini kwa dhamira waliyofanya. Kwa mbali, haikuwa nzuri ya kutosha. Tuliruhusu nafasi nyingi sana.

"Lazima uwe na njaa, lazima utoe kila kitu, kila mchezo, nadhani mchezo wetu wa kushambulia haukuwa mzuri, sitaki kuzingatia mtu mmoja.

"Haihusiani na mtu mmoja. Ilihusu utendaji wa timu. Hatukuivunja. Haikuwa nzuri vya kutosha."

"Hii ni kawaida," aliongeza. "Katika msimu, una vikwazo na unapaswa kukabiliana navyo mara nyingi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,099,1

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 05,06 NA 07 APRILI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/04/23 | 21:15 | Perugia vs Reggina | 2.52 | 2.94 | 2.83 |
| 02. 05/04/23 | 21:45 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 2.29 | 3.60 | 2.90 |
| 03. 05/04/23 | 22:00 | Barcelona vs Real Madrid | 2.29 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 05/04/23 | 22:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.25 | 2.22 |
| 05. 06/04/23 | 01:00 | Danubio FC vs SC Emelec | 2.38 | 3.05 | 2.84 |
| 06. 06/04/23 | 02:00 | Huachipato vs Union Espanola | 2.40 | 3.21 | 2.69 |
| 07. 06/04/23 | 04:05 | Pumas De Tabasco vs Zacatepec | 2.89 | 3.36 | 2.19 |
| 08. 06/04/23 | 05:00 | Deportivo Pereira vs Colo Colo | 2.58 | 3.08 | 2.58 |
| 09. 06/04/23 | 19:00 | Slask Wroclaw vs GKS Piast Gliwice | 2.43 | 3.09 | 2.67 |
| 10. 06/04/23 | 22:15 | El Ittihad Alexandria vs Coca Cola | 2.86 | 2.91 | 2.56 |
| 11. 07/04/23 | 03:00 | FBC Melgar vs Olimpia Asuncion | 2.25 | 3.13 | 2.98 |
| 12. 07/04/23 | 03:00 | CA Tigre vs Sao Paulo | 2.54 | 3.06 | 2.64 |
| 13. 07/04/23 | 08:00 | Western United vs Central Coast Mariners | 2.68 | 3.26 | 2.47 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# POTTER AFUKUZWA CHELSEA BAADA YA MIEZI SABA

**LONDON, England**

CHELSEA imemtimua kocha wake mkuu, Graham Potter Jumapili baada ya kuifundisha kwa chini ya miezi saba.

Chelsea ilichezea kichapo cha mabao 2-0 Jumamosi nyumbani kwa Aston Villa, kipigo cha 11 kwa Potter katika mechi 31 tangu kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel mnamo Septemba mwaka jana.

Ilithibitishwa kuwa Bruno Saltor, kocha ambaye aliondoka Brighton na Potter na kujiunga na Chelsea baada ya kuteuliwa, ataiongoza timu hiyo kama kocha mkuu wa muda.

Katika taarifa, wamiliki wa pamoja Todd Boehly na Behdad Eghbali walisema: “Kwa niaba ya kila mtu kwenye klabu, tunataka kumshukuru Graham kwa dhati kwa mchango wake kwa Chelsea.

“Tuna heshima ya hali ya juu kwa Graham kama kocha na kama mtu. Daima amekuwa akijiendesha kwa weledi na uadilifu na sote tumesikitishwa na matokeo haya.

“Pamoja na mashabiki wetu wa ajabu, sote tutakuwa nyuma ya Bruno na timu tunapoangazia msimu uliosalia. Tumebakiza michezo 10 ya Ligi Kuu na robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Tutaweka juhudi na kujitolea. katika kila moja ya mechi hizo ili tuweze kumaliza msimu kwa kasi.”

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba uamuzi wa kumuondoa Potter ulichukuliwa na Wakurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Paul Winstanley na Laurence Stewart, lakini kwa msaada kamili wa bodi.

Potter aliambiwa habari hizo katika mazungumzo ya ana kwa ana kwenye kambi ya mazoezi ya klabu ya Cobham juzi, Jumapili na vyanzo vimeeleza kuwa maelewano yalifikiwa kuhusu malipo yake, ikimaanisha kuwa atapokea chini ya thamani kamili ya mkataba wake katika masharti ya kukatwa.

Kipigo cha Jumamosi kutoka kwa Villa kiliiacha Chelsea katika nafasi ya 11 kwenye ligi ikiwa na tofauti mbaya ya mabao baada ya jioni nyingine kali ambapo mashabiki wa Stamford Bridge waliimba “Hujui unachofanya”.

# Pique aionya Barca kumrudisha Messi


**BARCELONA, Hispania**

GERARD Pique amewaonya Barcelona kwamba kumlazimisha Lionel Messi kurejea Camp Nou kunaweza “kutokuwa na tija”.

Messi anakaribia mwisho wa mkataba wake wa miaka miwili na Paris Saint-Germain, baada ya kujiunga na wababe hao wa Ligue 1 wakati shida ya kifedha ilipomlazimu kuondoka Barca mwaka 2021.

Mustakabali wa mshindi huyo wa Kombe la Dunia haujulikani, huku Barca wakihusishwa mara kwa mara na kutaka kumsajili mfungaji bora wa muda wote, huku Inter Miami inayomilikiwa na David Beckham pia wakitaka kumvutia Ligi Kuu ya Mareakani, MLS.

Wakati Kocha Mkuu wa PSG, Christophe Galtier, akifichua kuwa klabu hiyo inapanga mazungumzo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, Makamu wa rais wa Blaugrana, Rafael Yuste alikiri “napenda” kumuona fowadi huyo akirejea Camp Nou.



Pique, ambaye alitangaza kustaafu soka mapema msimu huu, alishinda mataji nane ya LaLiga na Messi akiwa Barca, pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu na Klabu Bingwa Dunia mara tatu.

Lakini beki huyo wa zamani anasisitiza kwamba muunganiko unaowezekana kati ya klabu yake ya zamani na mchezaji-mwenza lazima ufanyike kwa kawaida.

“Anamfahamu Yuste na ni mtu mzuri ambaye atakuambia kila wakati kile unachotaka kusikia,” Pique alisema wakati wa mahojiano na Gerardo Moreno. “Kulazimisha hali, kunaweza kutokuwa na tija. Mambo lazima yaende kawaida. Ikibidi kufanywa, itafanyika. Wakati kuna nia ya pande zote mbili, operesheni katika soka inaweza kufanikiwa kila wakati.”

# MAYELE: YANGA SC ITATUA NUSU FAINALI MICHUANO CAF

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Fiston Mayele, amesema uwapo wa kikosi bora katika timu hiyo kunampa imani kubwa ya kufanya vizuri michezo miwili ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na kutinga nusu fainali ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani humu baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Aidha, amesema kitendo cha Yanga kufanikiwa kupata pointi kwenye michezo ya ugenini na nyumbani ni ishara nzuri na ubora wa kikosi cha timu hiyo na anaamini kitasonga mbele zaidi katika mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jana ikiwa ni baada ya timu hiyo kuibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini nchini DR Congo dhidi ya TP Mazembe, Mayele alisema malengo yao makubwa yalikuwa ni kucheza makundi jambo ambalo limefanikiwa na kufika hatua ya robo fainali.

Alisema kwa mafanikio hayo ni ishara kubwa kwa Yanga kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao na anaimani kubwa ya watacheza nusu fainali.

"Malengo yalikuwa ni makundi, lakini tumevuka huko na sasa tunaenda robo fainali, hii ni ishara nzuri kwetu kufanya vizuri na kucheza nusu fainali kwa sababu ya ubora wa kikosi cha timu pamoja na aina ya wachezaji tuliokuwa nao," alisema Mayele.

Aliongeza kuwa wanatambua umuhimu wa michezo iliyopo mbele yao na watafanikisha kila lengo walilojiwekea na nguvu sasa wanazielekeza katika michezo iliyopo mbele yao hasa huo wa robo fainali.

"Sasa tumerejea nyumbani kujiandaa na michezo iliyopo mbele yetu ya Kombe la Shirikisho la Azam (FA Cup) na ligi kabla hatujacheza michuano ya kimataifa ya hatua ya robo fainali," alisema Mayele akidai ameumia kwa kitendo cha kutotetema katika ardhi yao ya nyumbani.

Alisema mama, baba na marafiki zake wote walikuwa uwanjani kwa ajili ya kumsapoti, lakini akashindwa kufanya kile alichokitarajia kwa kushindwa kufunga katika ardhi ya nyumbani kwao.

"Unajua nimecheza hii mechi nikiwa nimechoka kwa sababu nimetoka kwenye timu ya taifa, sikupata muda wa kumpumzika kikubwa tumepata ushindi na kuongoza kundi," alisema Mayele.

Kikosi cha Yanga kilirejea nchini jana jioni na wachezaji wamepewa mapumziko ya siku tatu kabla ya Alhamisi wiki hii kuingia kambini kujiandaa na mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Geita Gold FC utakaopigwa Azam Complex, Chamazi.

# Yanga mdomoni mwa Pyramids robo fainali

INATOKA UK. 24

timu kwani zote ni nzuri na inabidi ucheze nazo.

"Ukifika kwenye hatua hii huwezi kuchagua mpinzani kwa sababu timu zote ni nzuri na hata ukichagua, ukipita ile ambayo hujaichagua utakutana nayo, kwa hiyo sisi yeyote yule tukikutana naye sawa tu, huu siyo tena muda wa kucha-



gua mpinzani," alisema Kaze.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema hawakucheza vizuri dakika 45 za kwanza na dakika 10 za kipindi cha pili hasa eneo la katikati kwenye kiungo.

"Ni furaha kwenye klabu yetu ni kweli hatua ya makundi rekodi zinaonesha hatujawahi kushinda ugenini, lakini sasa tumefanya hivyo, na ushindi huu umetupatia kujiamini na mbinu ya nini tufanye kwenye mechi zijazo tutakapokwenda ugenini.

"Kipindi cha kwanza hatukuwa vizuri, na dakika 10 za kipindi cha pili, hasa katikati ndiyo maana tulimuingiza Farid Mussa aende kucheza namba kumi, halafu tukachezesha viungo wakabaji wawili kwa sababu tuliona pale mbele ya mabeki wa kati wanakosa watu wa kuwalinda," alisema.

Timu zingine zilizoongoza makundi yao ni Marumo Gallants ya Afrika Kusini ambayo ni kinara wa Kundi A, ASEC Mimosas (Ivory Coast) kinara wa Kundi B na FAR Rabat ya Morocco iliyokaa kileleni mwa Kundi C.

Kwa upande wa Marumo Gallants yenyewe hatua ya robo fainali inaweza kukutana na Pyramids, Rivers United ama US Monastir, wakati ASEC Mimosas ikiwa na uwezekano wa kukutana na Pyramids, USM Alger ama US Monastir huku FAR Rabat wapinzani wao wajao katika hatua hiyo wakitarajiwa kuwa USM Alger, Rivers United ama US Monastir.



# Robertinho aitoa hofu Simba CAF

INATOKA UK. 24

kuongeza:

"Simba ni timu kubwa na inacheza michuano mikubwa, kwa sasa tunasubiri droo na tumejipanga kucheza na yeyote tutakayepangwa naye katika hatua ya robo fainali," alisema Robertinho.

Alisema umakini mkubwa walionao kwa sasa ni kutumia michezo mitatu, miwili ya ligi na mmoja wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, kujiandaa na mechi mbili za robo fainali.

Simba leo wanaanza mazoezi na kuingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa ASFC dhidi ya Ihefu utakaopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.


164,188/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/04/23 | 17:00 | Fulham FC vs West Ham United | 2.55 | 3.15 | 2.60 |
| 02. 08/04/23 | 17:30 | Sampdoria Genoa vs US Cremonese | 2.24 | 3.10 | 3.10 |
| 03. 08/04/23 | 19:30 | Hellas Verona vs Sassuolo Calcio | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 04. 08/04/23 | 19:30 | Torino FC vs AS Roma | 3.15 | 2.95 | 2.31 |
| 05. 08/04/23 | 21:45 | Lazio Rome vs Juventus Turin | 2.60 | 2.90 | 2.80 |
| 06. 08/04/23 | 21:45 | KAA Gent vs Union Saint-Gilloise | 2.46 | 3.35 | 2.60 |
| 07. 09/04/23 | 14:00 | Olympique Lyon vs Stade Rennes | 2.25 | 3.30 | 2.90 |
| 08. 09/04/23 | 15:00 | Real Valladolid vs RCD Mallorca | 2.47 | 2.90 | 2.95 |
| 09. 09/04/23 | 15:30 | FC Emmen vs NEC Nijmegen | 2.80 | 3.30 | 2.35 |
| 10. 09/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.90 | 2.65 |
| 11. 09/04/23 | 16:00 | Montpellier HSC vs Toulouse FC | 2.28 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 09/04/23 | 16:00 | ESTAC Troyes vs Clermont Foot 63 | 2.55 | 3.20 | 2.60 |
| 13. 09/04/23 | 16:30 | Borussia Monchengladbach vs VfL Wolfsburg | 2.26 | 3.50 | 2.75 |
| 14. 09/04/23 | 18:30 | Liverpool FC vs Arsenal FC | 2.46 | 3.45 | 2.55 |
| 15. 09/04/23 | 18:30 | VfL Bochum vs VfB Stuttgart | 2.85 | 3.20 | 2.34 |
| 16. 09/04/23 | 19:30 | UD Almeria vs Valencia CF | 2.75 | 3.15 | 2.43 |
| 17. 09/04/23 | 19:30 | Standard Liege vs KRC Genk | 2.70 | 3.45 | 2.32 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 04/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4888 | Leixoes SC U23 vs Portimonense U23 | 2.37 | 3.47 | 2.56 |
| 14:00 | 2418 | Cardiff City U21 vs Sheffield Wednesday U23 | 1.43 | 4.78 | 5.19 |
| 14:00 | 3779 | Sukhothai FC vs Chonburi | 2.88 | 3.34 | 2.16 |
| 14:00 | 5630 | Chiangrai Utd vs Port FC | 2.61 | 3.23 | 2.40 |
| 14:30 | 1509 | Muang Thong Utd vs Lamphun Warrior | 1.55 | 3.84 | 4.92 |
| 14:45 | 1290 | Almopos Arideas vs Panathinaikos B | 2.42 | 2.70 | 2.85 |
| 14:45 | 3689 | Thesprotos vs Makedonikos FC | 4.23 | 2.94 | 1.91 |
| 15:00 | 1088 | Wolkite City FC vs Bahir Dar Kenema FC | 2.52 | 2.80 | 2.90 |
| 15:00 | 1833 | Bristol City U23 vs Sheffield United U23 | 2.47 | 3.73 | 2.34 |
| 15:00 | 3608 | Bangkok Utd vs Buriram Utd | 2.97 | 3.28 | 2.13 |
| 16:30 | 2949 | Persib Bandung vs Persis Solo | 1.47 | 3.90 | 4.90 |
| 17:00 | 3105 | Terengganu vs Kelantan FA | 1.25 | 5.15 | 8.85 |
| 17:00 | 3657 | Selangor FC vs Negeri Sembilan | 1.61 | 3.76 | 4.53 |
| 17:00 | 4667 | Ural Yekaterinburg vs Spartak Moscow | 2.80 | 3.16 | 2.34 |
| 17:00 | 5580 | Perak FA vs Johor Darul Takzim | 20.56 | 7.40 | 1.08 |
| 17:30 | 3010 | Varnsdorf vs Dukla Prague | 2.17 | 3.08 | 3.08 |
| 18:00 | 2588 | FC Hegelmann Litauen Kaunas vs FK Panevezys | 2.57 | 3.09 | 2.52 |
| 18:00 | 5604 | Futbolo Akademija Siauliai vs Zalgiris | 4.73 | 3.54 | 1.62 |
| 19:00 | 1066 | UTA Arad vs U Craiova SA | 2.63 | 2.94 | 2.63 |
| 19:00 | 3641 | Eintracht Frankfurt vs Union Berlin | 2.30 | 3.17 | 3.23 |
| 19:30 | 4595 | Dinamo Moscow vs Akron Tolyatti | 1.35 | 4.47 | 7.28 |
| 19:45 | 4263 | Maccabi Netanya vs Hapoel Katamon | 1.98 | 3.19 | 3.45 |
| 20:00 | 1505 | Hapoel Beer Sheva vs FC Ashdod | 1.50 | 3.86 | 5.36 |
| 20:00 | 5133 | Helsingborg vs Osters IF | 2.11 | 3.46 | 3.25 |
| 20:30 | 2206 | Maccabi Tel Aviv vs Maccabi Haifa | 2.12 | 3.24 | 3.03 |
| 20:30 | 4449 | Mamelodi Sundowns vs Cape Town City | 1.45 | 3.97 | 6.69 |
| 20:30 | 5527 | Ankaragucu vs Trabzonspor | 3.16 | 3.42 | 2.03 |
| 21:00 | 1779 | SV Spakenburg vs PSV Eindhoven | 10.45 | 6.69 | 1.17 |
| 21:00 | 4000 | Zalaegerszegi TE vs Puskas Akademia | 2.59 | 3.22 | 2.48 |
| 21:15 | 4878 | FC Basel vs BSC Young Boys | 2.87 | 3.44 | 2.12 |
| 21:30 | 4165 | KKS 1925 Kalisz vs Legia Warszawa | 7.44 | 4.65 | 1.33 |
| 21:45 | 1202 | Gateshead vs Yeovil | 1.61 | 3.82 | 4.92 |
| 21:45 | 1970 | Southport vs Banbury United | 2.18 | 3.20 | 3.05 |
| 21:45 | 2174 | Bayern Munchen vs SC Freiburg | 1.32 | 5.31 | 8.85 |
| 21:45 | 3346 | Bournemouth vs Brighton | 5.60 | 4.00 | 1.51 |
| 21:45 | 3402 | Chippenham Town vs Farnborough Town | 2.95 | 3.15 | 2.25 |
| 21:45 | 3722 | Stirling vs Elgin City | 1.48 | 4.06 | 5.34 |
| 21:45 | 3844 | Peterborough Sports vs Scarborough Athletic | 2.14 | 3.26 | 3.06 |
| 21:45 | 4339 | Leicester vs Aston Villa | 2.41 | 3.26 | 2.71 |
| 21:45 | 5086 | Stratford Town vs Redditch United | 2.49 | 3.37 | 2.49 |
| 21:45 | 5143 | Needham Market vs Barwell | 2.43 | 3.37 | 2.55 |
| 21:45 | 5653 | Farsley Celtic vs Brackley Town | 3.53 | 3.27 | 1.96 |
| 21:45 | 5734 | Raith Rovers vs Hamilton | 1.74 | 3.60 | 4.12 |
| 21:45 | 5892 | Leeds vs Nottingham | 1.78 | 3.45 | 4.20 |
| 22:00 | 2400 | Chelsea vs Liverpool | 2.38 | 3.34 | 2.69 |
| 22:00 | 2782 | Athletic Bilbao vs Osasuna | 1.58 | 3.62 | 5.66 |
| 22:00 | 3193 | Juventus vs Inter | 2.37 | 3.15 | 2.99 |
| 22:00 | 3254 | Weston Super Mare vs Winchester City FC | 1.29 | 5.18 | 7.45 |
| 22:15 | 1854 | Aswan vs Smouha Club | 2.72 | 2.87 | 2.72 |
| 22:15 | 2675 | El Daklyeh vs Farco FC | 2.61 | 2.66 | 3.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Aprili 4, 2023
Nipashe



UKURASA 21

**Ten Hag akubali United ilistahili kipigo Newcastle**

# YANGA SC MDOMONI MWA PYRAMIDS

## Ikikwepa kuangukia kwa USM Alger ya Algeria ama Rivers United ya Nigeria, yatamba waleteni, Mayele naye asema...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI droo ya hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika ikitarajiwa kuchezeshwa kesho, Jumatano jijini Cairo Misri, miamba ya Tanzania katika michuano hiyo, Klabu ya Yanga itakutana na moja kati ya timu hizi tatu, Pyramids ya Misri, USM Alger ya Algeria ama Rivers United ya Nigeria.

Yanga imetinga hatua hiyo baada ya kuongoza Kundi D ikiwa na pointi 13 sawa na US Monastir ya Tunisia, lakini mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara, wakiwazidi Watunisia hao kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Yanga imemaliza kundi ikiwa kinara na hii ni baada ya juzi usiku US Monastir kuifunga Real Bamako ya Mali mabao 2-1 huku yenyewe ikishinda 1-0 ugenini dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo.

Yanga inaongoza kwa tofauti ya bao moja, zote mbili zikiwa na pointi 13, ina mabao tisa, huku US Monastir ikiwa na mabao manane.

Kwa mujibu wa kanuni za michuano hiyo, mshindi wa kila kundi atakutana na moja ya timu tatu zinazoshika nafasi ya pili katika makundi mengine matatu, hivyo kuifanya Yanga kusubiri moja kati ya Pyramids, USM Alger ama Rivers United.

Hata hivyo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, ambaye juzi aliongoza timu hiyo kuhitimisha hatua ya makundi kwa ushindi huo wa ugenini dhidi ya TP Mazembe, amesema hawaogopi kucheza na timu yoyote ambayo watapangwa nayo kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Kaze alisema kwenye hatua ambayo wamefika huwezi kuchagua

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akimtoka beki wa TP Mazembe, Youssifou Atte, kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa TP Mazembe, Lubumbashi nchini DR Congo juzi na wageni kushinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Robertinho aitoa hofu Simba CAF

**Na Saada Akida**

HUKU Shirikisho la Soka Afrika (CAF), likitarajia kuchezesha droo ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kesho, Simba imeweka wazi kuwa wako tayari kukutana na timu yoyote watakayopangwa nayo.

Timu nane zilizofanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali ni CR Belouizdad (Algeria), Esperance Tunis (Tunisia), JS Kabylie (Algeria), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Raja Casablanca (Morocco), Wydad AC (Morocco), Al Ahly (Misri) na Simba (Tanzania).

Kutokana na kanuni za mashindano hayo, mshindi wa kwanza kutoka katika kila kundi kukutana na mmoja aliyeshika nafasi ya pili kutoka makundi mengine matatu, Simba inaweza kukutana na Wydad AC, Mamelodi Sundowns ama Esperance Tunis ambazo ni vinara wa makundi yao.

Simba wamefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali baada ya kukusanya pointi tisa katika Kundi lao la C, linaloongozwa na Raja Casablanca iliyomaliza na alama 16.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, aliwatoa hofu mashabiki wa miamba hiyo, akisema timu hiyo ni kubwa na imekuwa katika nafasi nzuri, hivyo hana cha kuhofia katika hatua inayofuata ya robo fainali.

Alisema kazi kubwa iliyopo kwa benchi la ufundi ni kuandaa kikosi chao kuwa imara na hawana hofu ya mpinzani watakayekutana naye kwa sababu Simba ni timu kubwa na iko katika mashindano makubwa.

"Kama nilivyosema awali kuwa malengo yangu ni kuona Simba inafikia malengo yao ya kucheza robo na sasa wanafikiria kucheza nusu fainali ya michuano hiyo, nguvu zetu tutazitumia katika michezo hii mitatu kujiandaa na mechi mbili za robo fainali," alisema Robertinho na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >